# *Ubatizo Wa Maji*

Naam. . .Vema, sasa, mawazo ye—yetu asubuhi ya leo ni kwamba, hatutaki ku—kuchukua muda wenu mwingi kupita kiasi, lakini basi nina. . .nami niende nikasome kidogo, ndipo nitakuwa tayari karibuni sana kuninii. . . Sina budi kwenda kwenye chakula cha kutwa leo hii pamoja na watu fulani, nami niliwazia kabla mambo mengi sana hayajalundikana. . .Kuna mama mhudumu anayekuja kutoka hapa juu, dada ya Ndugu Jack Moore, ambaye anataka kuzungumza nami kuhusu wahubiri wanawake. Nami najua atakuwa humu leo hii, basi niliwazia ningefika huku kwanza.

2 Na mimi. . .jambo la kwanza ninalowatakeni nyote mjue (Huu unarekodiwa, Leo?), hilo hapo jambo la kwanza ninalowataka ninyi nyote mjue, mnaona. . .Na hao ni Dada Gibson na Dada Sewell na Dada Simpson. Mnaona? Niliulizwa swali kuhusu ubatizo wa maji, nami. . .mnataka kujua kuuhusu. Ni—ningewataka ninyi nyote mjue kwanza, kwamba nina ninii. . .lengo langu si kujaribu kuonyesha, kana kwamba ulikuwa ni mwanzilishi ama ulijua zaidi ya mtu mwingine. Lengo langu ni kujaribu kuelezea, kadiri nijuavyo mimi kwa Maandiko, yaliyo kweli na uongo. Na sikuzote limekuwa lengo langu kutopatana juu ya lolote ambalo Mungu ameandika, wala nisiseme kwamba ni la kweli kwa sababu mtu mwingine anasema ni la kweli. Lakini linapaswa kuwa hivyo.

3 Sasa, huenda ikawa ni hivi, kwamba katika siku za usoni kama mngeisikiliza kanda hii ambayo tunazungumzia, huenda ikawa ni jambo jema nikiwaambia sababu yake. (Nyote mnaweza kunisikia vizuri vya kutosha?) Ninii. . .

4 Ninafikiri Baba yetu wa Mbinguni anao watu walioumbwa kwa njia fulani kwa faida Yake Mwenyewe. Ni kama tu vile tunavyofanya mambo kwa njia fulani, tofauti kila wakati, kwa sababu tuna kusudi la kufanya hivyo.

5 Wakati fulani uliopita nilikuwa nimeketi chini katika—katika jimbo la Kentucky nikizungumza na baadhi ya ndugu zangu, na. . .Ninapoenda nyumbani na ninaweza kupata wakati mdogo kutoka kwenye mikutano, kwa kawaida kuna umati mkubwa unaokusanyika. Mnaona? Ndipo ninashikwa na wasiwasi sana, baada ya usiku kucha, mnaona, hupumziki hata kidogo; wanakuja tu usiku na mchana; ninashikwa na wasiwasi kweli. Ndipo ama nitachukua ufito wangu wa kuvulia niende kuvua samaki, ama endapo ni msimu wa kuwinda, nitaichukua bunduki yangu niende kuwinda.

6 Vema, bunduki ni moja ya vitu ninavyopenda kujipumbaza kwavyo; kulenga shabaha. Ndugu Gene, hapa, na mimi, ameanza

kutia risasi kwa mkono sasa, nasi... tunapenda tu kufanya hivyo.

7 Halafu nilikuwa na maskini, ile wanayoita Muundo 75, bunduki ya Winchester .22; vema, hiyo ndiyo ninayowawindia kuchakulo. Vema, mimi—mimi huwawinda kuchakulo kwenye umbali wa yadi hamsini. Na kwenye yadi hamsini... ninaendelea kuchezacheza na maskini bunduki hii ndogo mpaka ninaweza kulenga shabaha nayo kwenye yadi hamsini. Na hivi majuzi nilipiga risasi tisa katika shimo lile lile (Hiyo ni kweli, Ndugu Gene?) kwenye yadi hamsini, kwa bunduki ya .22. Sasa, vema, mara ikaenda kombo.

8 Sasa, kwa kawaida kama kuchakulo ananiangalia, sitampiga risasi. Kama amenipa kisogo, sitampiga risasi. Inampasa kuwa ameketi kusudi niweze kuliona jicho lake. Na ikitokea nimpige chini ya jicho, ama juu ya jicho, ninajua bunduki yangu ina kasoro, mnaona. Kwa hiyo nitaninii tu... sijaribu kujidanganya, nami ninaninii tu... Wala siwachukui kuchakulo zaidi ya wale sheria inaoniruhusu kuwachukua (Mnaona?), maana hilo ni sahihi; mimi ni mhifadhi.

9 Lakini ninaninii tu... Nikimwona mmoja na yuko mbali sana, ninaachana tu naye. Na kama huyu yuko karibu sana nami, nitarudi nyuma kwenye yadi hamsini. Nami nitamwangalia akitoka kwenda kuchukua kokwa la hikori kisha arudi, yeye ananiangalia, ninaachana tu naye. Wakati mwingine anapopata nyingine labda dakika kumi baadaye, baada ya kuipasua hiyo, ataenda achukue moja, labda amegeuza mgongo wake; nisingempiga risasi namna hiyo. Kwa hiyo, na kama akiondoka, vema, acha aende; nitajiwindia mwingine (Mnaona?), maana ninaninii tu—ninawatafuta tu.

10 Nami nawapenda. Ndio nyama iliyo nzuri sana iliyopo ulimwenguni; hakuna kitu cha kulinganisha na kuchakulo wa kijivu, hasa sana wakati anapokata mfume, ama hikori, ama kitu kama hicho.

11 Kwa hiyo bunduki yangu ikaenda kombo. Sasa, bunduki ni kitu cha ajabu kujipumbaza nayo. Ni—ni kitu kinachoniondolea mkazo kwenye mishipa yangu na kadhalika. Sasa, watu wengine wasingeijali.

12 Nami ninaamini ndugu yetu mwenye fadhili Oral Roberts, nafikiri yeye hucheza gofu, na vivyo hivyo ndugu yetu Billy Graham. Wao hucheza gofu. Hiyo ingesumbua fahamu zangu, kuwa huko nje pamoja na hao wanawake walio nusu uchi na kadhalika, kule. Nisingeweza kustahimili hilo, ni lile wazo... Lakini sasa, labda, hao ndugu... Simaanishi wanatoka kwenda huko nje kwa kusudi hilo, mnaona. La, kwa sababu wao ni—wao ni—wao ni waungwana, wao ni ndugu Wakristo. Lakini kutoka tu kwenda karibu na hapo, nisingeweza kuvumilia hilo, mnaona. Inafa-...

13 Na kucheza gofu, mimi—mimi . . . hiyo inaonekana kwangu kama kwamba ni ya—ni ya wanawake, ama kitu fulani, mnaona. Kuupiga mpira kwa kijiti kisha kukimbia kule. Sasa, hao ndugu huenda wakawazia jambo lile lile: "kuketi kitako, kujipumbaza na bunduki ya kale." Vema, mnajua tumeumbwa tofauti.

14 Na kwa hiyo bunduki hii, mtetemeko ulio mdogo sana wa namna yoyote, utaikosesha shabaha. Unaweza kuwa ukipiga risasi na kulenga shabaha nayo, kisha uweke kidole chako kwenye mtutu, ita—itaharibu tu shabaha yako, unaona. Hivyo ndivyo hiyo . . . jinsi inavyopaswa kuwa sahihi. Huwezi kuuzungusha mkono wako kwenye kiganja cha mkono; uisawazishe mkononi mwako.

Ndipo basi mnasema, "Hayo yote yana uhusiano gani na yale tunayokuuliza?" Lakini ninajaribu kuwafikisha kwenye jambo fulani kwanza, kupata msingi.

15 Sasa, siku moja ilienda kombo, nami nilikuwa nimefanya kila kitu nilichojua jinsi ya kufanya kuifanya . . . kuirejesha tena. Nikajaribu kuikarabati. Nikajaribu kuikaza, kuilegeza, na kadhalika.

16 Nayo ya .22 huwezi kuitia risasi kwa mkono, kwa kuwa fataki iko kwenye ganda nawe huna budi kuchukua risasi zilizoingiziwa kiwandani. Sasa, mahali tunapotia zile zilizo na ri—risasi kubwa, mahali tunapoweza kugonga fataki itoke na kuchukua kibadilisha ukubwa na kadhalika, vema, tu—tunaweza kuitia hiyo na kuendelea kubadilisha baruti, na gramu, na uzito wa risasi, mpaka tufikie ambapo itapiga risasi kile itakachopiga risasi, ama labda tuingie kwenye matandiko na kadhalika. Kwa hiyo tusingeweza kufanya hivyo kwenye hiyo. Lakini nikasema, "Vema, labda niliharibu matandiko. Nitairudisha kwa Kampuni ya Winchester."

17 Nikairejesha kwa Kampuni ya Winchester, nao wakaniandikia barua, ambayo ninaweka kwa ku—kumbukumbu yake tu. Wao wakasema, "Kasisi Branham, hii Winchester Muundo 70 haikuundwa iwe bunduki ya kulenga shabaha." Mnaona. Kasema, "Itaenda kombo inchi moja . . . lundo la risasi saba, itaenda kombo inchi moja kwenye yadi ishirini na tano." Kisha kasema, "Kamwe hutaifanya nzuri zaidi ya hivyo, maana hiyo ni kamilifu kwa bunduki ya aina hiyo; inchi moja kwenye yadi ishirini na tano."

18 Nilijua hilo halikuwa kweli. Nilikuwa tayari nimelenga risasi tisa, shimo moja katika ile nyingine, kwenye yadi hamsini nayo. Na hiyo ilikuwa ni Kampuni ya Winchester iliyoiunda.

19 Sasa, inaonekana kana kwamba mtu fulani angesema, "Vema, kama wahandisi walitoa amri ya kuiruhusia bunduki hiyo, nao wanapaswa kujua kilicho ndani yake, na kama wao waliiunda bunduki hiyo, basi mbona wewe . . . ?"

20 Hivyo ndivyo mke wangu alivyoniambia. Kasema, "Billy, kwa nini kujipumbaza na bunduki hiyo, baada ya watu waliyoibuni na kuiunda, na wanajua hata kiasi cha gesi iliyomo ndani ya kila risasi na kila kishikizo kilicho ndani yake na chochote kile, u—ungewezaje kujaribu kubishana na neno lao?"

21 Nikasema, "Vema, kipenzi, sio muda mrefu uliopita ulikuwa ukiniuliza swali la Biblia, nawe ulikuwa na majibu nyuma ya Biblia. Nawe ukaniuliza, 'Hivi Mungu alimpa Ibrahimu ile nchi ambayo Yeye alimwahidia?'" Na—na, ama, yeye aliniuliza.

Nami nikasema, "La, kamwe Yeye hakumpa hiyo nchi. Yeye alimwahidia, bali kamwe—kamwe hakurithi yoyote ya hiyo. Kamwe hakuipata."

Na kwa hiyo akasema, "Loo, nimekushika kwa hilo." Akasema, "Hili hapa jibu, 'Yeye alimpa hiyo.'"

22 Nikasema, "Fungua Matendo 7. 'Wala hakumpa hata kiasi cha kuweka mguu wake.'" Hiyo ni kweli, ha—hakupewa hiyo. Sasa, mnaona, wakati mwingine majibu yetu ya kujibunia yaliyoandikwa yanaweza kukosea.

23 Naye mtu anayeiunda bunduki anaweza kukosea, kwa sababu tayari ninajua nililenga risasi tisa moja kwa moja kwenye kipande cha karatasi katika shimo lile lile kwenye yadi hamsini kwa bunduki hiyo. Nao walisema kama risasi saba zinaninii. . .unachukua inchi moja kwenye yadi ishirini na tano, nusu ya umbali huo, usingeweza kuiboresha. Kwangu mimi wao walikosea, kama wao ndio mabingwa wa hiyo bunduki ama sivyo, maana nilijua vema zaidi, mnaona.

24 Ndipo niliketi chini ya mti asubuhi moja, naye Ndugu Wood na Ndugu Charlie, wanaowinda pamoja nami, na kulikuwako na kuchakulo kila mahali. Vema, nilikuwa nimempiga risasi mmoja siku kadhaa kabla ya hapo na kulikosa jicho lake; ikampiga chini kabisa ya shavu lake. Hakika, ilimwua kuchakulo huyo kadiri ingalifanya kama ingalimpiga kwenye jicho, lakini hiyo bunduki ilienda kombo, kwangu mimi. Inanitia fadhaa, maana iwapo bunduki hiyo si kamili kabisa, mimi—mimi. . .hainifai kitu kwenda kuwinda (Mnaona?), kwa maana siwindi kwa ajili ya nyama yake kwa vyovyote vile. Ni—ninawinda tu kwa kujifurahisha.

25 Na kwa hiyo nikasema, "Hiyo ni. . .Ni. . ." Nilikuwa nimeketi chini ya mti, mti mdogo ulioinama. Ningeweza kuuendea asubuhi ya leo, kule kwenye milima ya Kentucky. Basi nilikuwa nimeketi nyuma chini ya mti huo, nikimsikiliza Charlie hapa akifyatua-fyatua tu. Walikuwa. . .Sijali walipiga risasi upande gani wa kuchakulo, maadamu tu walimpiga risasi kuchakulo. Ninii yao. . .kama kundi lao. . .haidhuru bunduki yao ilikuwa ikilenga vyovyote, maadamu tu walimpiga risasi

kuchakulo. Na endapo i—ilikuwa kwenye nyonga, ama katikati, ama popote pale ilipompiga, hiyo ilikuwa ni sawa.

26 Na kwa hiyo . . . nami nikasema, "Vema, sasa, hilo halininii . . ." Ka—kamwe nisingestahimili hilo. Ndipo nikaketi pale chini. Nikawazia, "Hebu angalia tu jinsi hao jamaa wanavyojifurahisha." Nao wanapenda kuwinda sawasawa na mimi, nao wote wawili wana shabaha nzuri, bora sana. Wao ni watu wazuri sana, wote wawili ni Wakristo, waliojazwa na Roho Mtakatifu, nao ni watu wazuri tu; baadhi ya watu walio wema sana. Nao hao ndugu huko juu walikuwa wakijifurahisha sana, wakipiga kuchakulo risasi. Na kulikuwako na kuchakulo waliokuwa wakiruka mitini karibu sana nami.

27 Vema, nikasema, "Basi kwa nini nifanye jambo kama hilo? Nikaketi hapa, nami huyu hapa nimeketi hapa nikilia, machozi tu yakitiririka usoni mwangu. Hao hapo, na hapa siwezi hata kupiga shabaha." Basi nikasimama na kusema, "Baba wa Mbinguni, kwa nini ukaniumba namna hii, maskini mtu mwenye wasiwasi, mwenye fadhaa? Halafu neema Yako imenipa mamilioni hasa ya marafiki," mnaona. Ndipo nikasema, "Kwa nini unifanye mtu wa namna hii?" Ndipo nikaanza kulia kwa sauti kuu basi, nimeketi chini ya mti mdogo ulioinama, papo hapo, chini ya mlima.

28 Na—nami nilijua, karibuni jamaa hao wangepata kiwango chao cha kuchakulo, na kurudi. Nami huyo hapo nimeketi pale, ninii tu . . . Loo, haikuwa . . . lakini ka—kamwe sikuwa na ujasiri wa kumpiga risasi mmoja wao, maana, nilihofu ningemdhuru, mwajua, naye a—atoroke, mnaona.

29 Nami nikaniii tu . . . nayo bunduki yangu, ningeninii . . . Msimu si mrefu sana, na nilikuwa wakati huo, kwa kuwa, vema, nusu ya msimu ilikuwa imekwisha nikijaribu kuikarabati bunduki hiyo. Nilituma darubini, ikachunguzwe, nao wakasema, "Darubini ni barabara kabisa."

30 Vema, nilijua ilikuwa ni bunduki, maana inarusha moja, upande mmoja, na nyingine, mwingine. Ni vigumu kwa darubini kufanya hivyo. Kwa hiyo niliketi chini pale na ni—nikalia tu.

31 Na baada ya kuketi pale muda kidogo, kwa namna fulani nikakishikilia kichwa changu, nilimsikia Yeye akizungumza nami. Sasa, nyote mlisimama jana usiku mikutanoni; mkaona vile Yeye angeenda kwenye kusanyiko, popote pale, popote aliponitaka, akawaambia watu yote kuhusu hali zao, na kwamba walikuwa ni akina nani, na mahali walipotoka, na yale waliyokuwa wamefanya, na yale yatakayotukia. Mliwahi kuona hilo likishindwa? Kamwe halishindwi; haliwezi, maana ni Yeye. Vema, basi, Yeye alikuwa akizungumza nami. Naye akasema—Yeye akasema, "Nilikuumba hivyo kwa kusudi fulani."

32 Nami nikasema, "Kwa nini ukaniumba hivyo, Bwana, kwa kusudi fulani, kuwa na wasiwasi? Na kitu pekee cha

kuniburudisha kutoka kwenye mikutano ni kuja hapa na kuwinda. Na Wewe ungeniruhusu . . . " Mnaona, Mungu hufanya kila kitu kitende kazi vema kwa ajili ya hao wampendao, mnaona. Yeye alitaka kuniambia jambo fulani. Hivyo ndivyo ilibidi bunduki hiyo iende kombo, apate kunipasha jambo lili hili.

Akasema, "Vema . . . "

33 Nikasema, "Bunduki yangu," nikasema, "Bwana, Wewe Ndiwe pekee ungaliweza kuirekebisha." Nikasema, "Wewe Ndiwe pekee ungeweza kunisaidia, kwa sababu Kampuni yenyewe ya Winchester inasema ya kwamba haitalenga ila inchi moja katika yadi ishirini na tano. Na, Bwana, ninaijua: Ni—nimepiga risasi kwenye yadi hamsini na kulenga risasi tisa moja kwa moja. Mnaona? Ninajua tofauti na hayo."

34 Akasema, "Hiyo ndiyo sababu nilikuumba namna hiyo." Kasema, "Unaona? Wewe . . . Nilikufanya jinsi hiyo kusudi . . . kwa kusudi fulani." Sasa, na hivi ndivyo ilivyokuwa. Mnaona? Kama nilijua ingeweza kulenga shabaha kwenye yadi hamsini, sijali ni nani anayesema vinginevyo, ninajua itafanya hivyo, kama inaweza kuwekwa katika hali nzuri; kama usawa, risasi, na ninii—na ninii . . . mienendo yote ya bunduki inaweza kuchunguzwa na kurekebishwa. Kwa maana ilifaulu wakati mmoja; kama ilifaulu wakati mmoja, itafaulu tena.

35 Vema, hapo ndipo aliponijulisha mimi, wakati huo, Yeye aliniumba hivyo kwa ajili ya lile agizo alilonipa Yeye kwa ajili ya siku hizi ninazoishi; kwamba siwezi kwenda tu kwenye kanisa la kimadhehebu na kujiunga na moja, wakati yatarusha tu takataka: "Vema, ka—kanisa linasema *hili* ni sawa nao wanakubali *hili*."

36 Iwapo—iwapo—iwapo Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama ililenga risasi pale, itailenga tena. Sijali wasemayo. Mnaona? Inabidi pawe na njia ya kwamba Yeye ni Mtu yule yule. Yeye ni kitu kile kile. Nguvu Zake ni zile zile.

37 Sasa, unapofikia mahali kama hapa, Mathayo 28:19, ambapo mnaniuliza asubuhi ya leo, Matendo 2:38. Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake hapa: "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka." Sasa, hiyo ni Marko 16, ndiko ninakonukuu. Na sasa, hapo ni wakati Yeye alipowaagiza. Wala hakutaja jinsi ya kubatiza mle ndani. Marko kamwe hakuliandika.

38 Lakini Mathayo alisema, Mathayo 28:19, Yeye alisema, wakati alipowatokea, halafu, kadhalika, akawaagiza waende wakabatize, Yeye alisema, "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote." Nayo tafsiri ya kweli ni kwamba, ni, "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza

katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru."

Ndipo siku kumi baadaye Petro akasema, "Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo." Sasa, hiyo hapo hitilafu dhahiri!

39 Sasa, karibu watu wote watasema, "Vema, kanisa langu hufundisha, 'Mkabatizwe, jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Seminari niliyotoka ilinifundisha hilo, kwa hiyo hivyo ndivyo nitakavyolifanya."

40 Kwangu mimi hiyo si haki. Ninapiga *hapa* na kupiga *pale*. Ninalenga sha—shabaha ya inchi arobaini. Hilo silo, haliyafanyi Maandiko sahihi. Halina budi kulenga kikamilifu. Halina budi kulenga kikamilifu. Vema, basi, yatalengaje kikamilifu wakati Mathayo alisema, "Mkabatize, jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," naye Petro akasema, "Mkabatize, Jina la Bwana Yesu," wote wawili wanafunzi, mmoja, mwandishi, na huyo mwingine, mtume?

41 Ndipo basi, kila mtu katika Biblia aliyebatizwa baada ya hapo, alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na wale ambao tayari walikuwa wamebatizwa na Yohana ilibidi waje wakabatizwe tena, katika Jina la Yesu Kristo, kabla hawajampokea Roho Mtakatifu.

42 Vema, nikasema, "Mnaona, ha—hamjalenga pale." Hili hapa jambo fulani sasa hivi. Kama tunaiamini Biblia kuwa ni Neno lisilokosea la Mungu, hatuwezi kulifanya lirushe matope kote kwenye kipande cha karatasi na kisha lilengwe kikamilifu. Mnanielewa? Halina budi kulenga shabaha, la sivyo haliipigi. Iwapo liko kombo, liko kombo.

43 Vema, kwa nini Petro akageuka na kufanya jambo ambalo Yesu alimwambia asilifanye? halafu Mungu alitambue na kuwapa Roho Mtakatifu, wakati—wakati Yesu aliposema, "Mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," naye Petro akasema, "La, batizeni katika Jina la—la Yesu."

44 Sasa, ha—hamwezi kulifanya hilo lilenge shabaha. Mnaona? Sasa, kuna kasoro mahali fulani, dada. Mnaona? Ama mmoja alisema uongo, ama ninii . . . Ni yupi aliyesema uongo? Alikuwa ni yupi? Sasa, kwangu mimi hilo kamwe halitafanya kazi.

45 Ni kama tu jinsi ilivyo kwa: "Ushahidi wa ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha, ama sivyo?" Wengine husema, "Naam," na wengine husema "La." Maandiko yanasema nini juu yake? Hayana budi kulenga kikamilifu! Ninaona pale, ambapo, wengine kweli walinena kwa lugha, na wengine hawakunena. Vema, ni kitu gani?

46 Swali lingine lililo muhimu sana: "Wanawake wanapaswa kuwa wahubiri, ndiyo, ama la?" Mahali fulani panasema, "Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu

na binti zenu watatabiri." Pengine palisema, "Simpi ruhusa, mwanamke kunena kanisani," hata. Mnaona?

47 Sasa, hilo halilengi kikamilifu. Halilengi kikamilifu, kwa hiyo wao. . .Kamwe usiliache tu jinsi hiyo kwa sababu seminari, kiwanda, kasema ilikuwa, ni, "Hilo ni zuri kadiri utakavyolipata." La, bwana. La, bwana. Halina budi kulenga shabaha, la sivyo halifai kitu. Vema, sasa kama lililenga kikamilifu kwa ajili yao, litalenga kikamilifu kwangu. Kama lililenga wakati mmoja na kuleta matokeo ya kudai ufufuo wa Yesu Kristo pamoja na nguvu na ishara na miujiza na maajabu, litafanya hivyo tena.

48 Sasa, mahali fulani tumeninii. . .tuna. . .tuna mikwaruzo mingi kupita kiasi kwenye mtutu. Mnaona ninalomaanisha? Hii ni njia fidhuli ya kulielezea, kuhusu kupiga risasi kwa bunduki, lakini ninaninii tu, ninafa-. . .ninaliweka hilo kama msingi mpate kufahamu ninalomaanisha. Kuna mkwaruzo kwenye mtutu mahali fulani; haujafungwa vizuri; baruti ama ni nyingi sana au ni kidogo sana; ama labda skrubu moja imekazwa sana na hiyo nyingine imelegea, au moja imelegea sana na hiyo nyingine imekazwa; na kuna kasoro mahali fulani. [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam, naam, naam, huenda ikawa ni jamaa aliye nyuma ya kifyatuliaji, yuko sahihi. Lakini sasa, ni kitu gani basi?

49 Sasa, kama kukiweko na kuhitilafiana katika Neno la Mungu kinagaubaga kama hapo palivyo, basi hilo si Neno la Mungu nilijualo. Kama anaweza kujichanganyisha Mwenyewe, na kulichanganyisha Neno Lake, na kujichanganyisha Mwenyewe, Yeye si asiye na kikomo, Yeye yuna kikomo kama nilivyo mimi.

50 Sasa, hiyo ni kweli? Neno hilo ama halina budi kuwa ni la kweli na kila sehemu Yake ni kweli na limelenga kikamilifu, ama la sivyo si Neno la Mungu.

51 Sasa, mara nyingi watu husema, "Vema, mnaona, Petro alikuwa ameshikwa na msisimko sana hapo aliposema mkabatize, Jina la Yesu, kwa sababu kwamba—kwamba, kweli, Mathayo alisema vile hasa Yesu alivyosema. Hatujali yale Petro aliyosema."

52 Vema, basi, kama Petro na Yesu hawakuafikiana, basi Injili zote huenda haziafikiani. Kama Neno moja la Hilo linapinga hilo lingine, basi si Neno la Mungu, la Mungu yule ninayemjua.

53 [Mtu fulani anasema, "Labda Yohana alifanya makosa fulani."—Mh.] Naam, huenda Yohana alifanya makosa. Ni yupi aliyekuwa sahihi? Hata hivyo iliku-. . .Sijui kama Yesu alisema hivyo ama la. Mnaona? Mathayo aliliandika. Marko kamwe hakusema lolote kulihusu, Luka kamwe hakusema lolote kulihusu, wala Yohana kamwe hakusema lolote kulihusu, bali

Mathayo alisema. Vema, basi labda Injili yote ya Mathayo ilikosea, na ya Luka. Vema, basi, ni ipi iliyo ya kweli na ipi ya uongo? Unaona mahali umejipeleka? La, bwana, Yote haina budi kuwa ni ya kweli.

54 Basi nashangaa, kwa nini Mungu kuandika Kitu kama hicho, na kukiacha kichanganyikane? Hata Yesu alimshukuru Baba Yake kwamba amelificha hili kutoka kwa macho ya wenye hekima na wenye elimu, na kuwafunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza. Sasa, limefanywa hivyo lipate kuwatupilia mbali we—we—wenye hekima. Lakini hiki Kitabu ni ufunuo.

55 Sasa, ni kama wakati ninapoenda katika nchi za ng'ambo naye mke wangu ananiandikia barua nami naketi chini. Yeye alisema, "Mpendwa Billy, nimeketi hapa usiku wa leo; watoto wamelala. Niliwazia ningekwandikia mistari michache kukujulisha yale tuliyofanya leo hii na jinsi tunavyoendelea. Tunatumaini ya kwamba Mungu anakubariki," na yote namna hiyo. Sasa, ninasoma kutoka mistarini yale yeye anayoandika. Lakini ninampenda sana mke wangu, naye ananipenda sana, haidhuru ningeandika nini, tunaweza kusoma katikati ya mistari kile tunachomaanisha.

56 Vema, hivyo ndivyo Biblia ilivyoandikwa: katikati ya mistari. Mnajua juu ya mengi ya mahubiri yangu, kama vile Mungu kuwarudisha Ibrahimu na Sara wakawa vijana, ingekubidi—ingekubidi kusoma katikati ya mstari kuona jinsi ambavyo, yale Maandiko yasemayo. Inakubidi kujua. Bali kamwe hayataenda nje ya mstari. Mnaona? Katikati ya mistari kutaileta tu hiyo mistari pamoja na kufanyiza picha moja kubwa.

57 Sasa, haina budi kuwa ni upendano na Mungu kabla hujaweza kulipata, maana Roho Mtakatifu aliiandika Biblia; nayo Biblia ilisema ya kwamba si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, bali imevuviwa.

58 Sasa, tuliendee swali lenu. Mna Biblia? Nyote mna Biblia? Sasa, kwanza. . . [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] La, hiyo ni sawa. Kama m—m—m—mnaweza kuliandika, ama kuninii tu. . . Sasa ninataka kuwapa mifano michache, kama hamtajali. Na katika jambo hili, basi, m—mtaona ni kwa nini. Sasa, ninataka kuwaulizeni ninyi dada swali.

59 Ninawatakeni mwe huru iwezekanavyo. Sasa, tudumu kwenye somo hili kwa ajili ya kanda hii, kwa sababu ninamaanisha ya kwamba tungeenda kombo juu ya ushahidi wa kwanza na kila kitu kingine namna hiyo. Lakini hebu. . . Tutanasa kanda nyingine kwa ajili ya hilo (Mnaona?) wakati mwingine. Lakini hili, tunazungumza juu ya ubatizo wa maji.

60 Sasa, inaonekana kana kwamba Mathayo na Petro, kama walikuwa wakilenga shabaha ile ile, walikuwa mbali sana na mstari mahali fulani.

61 Sasa, sasa nitachukua katika—katika Biblia yangu na nitasoma. Na—na ninyi dada, kama mkitaka kuisoma, iweni tu. . .mkitaka. . .mnataka Biblia ama mnataka kuliandika ama chochote zaidi, fanyeni tu mtakavyo. Kisha nitaninii—nitawapatia. . .Ninawatakeni ninyi basi ku—kuninii. . .mkiisha kufanya hivi, liandikeni. Halafu basi kukiweko na maswali yoyote, ninawatakeni mwe na hakika na—na kuniuliza sasa. Niulizeni, ili kwamba wakati wowote wa usoni, kwenye kanda hii, ambapo ingembidi mtu fulani kuwauliza swali, mwaweza kurudi na kulielezea.

62 Sasa, kusudi tuwanyoshe watu hawa na kuwaweka hawa wawili chini vizuri, na—nataka kuninii. . .itabidi. . .labda. . . karibu kuyaunganisha masomo mawili pamoja.

63 Sasa, sasa, katika Mathayo 28:19, sasa, hicho ndicho kitabu cha mwisho cha Biblia, ama, kitabu cha mwisho cha Mathayo, sehemu ya mwisho ya Mathayo. Sasa, hebu tusome vifungu vya mwisho, kifungu cha 18:

> *Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*

64 Vema, nashangaa kama, hivi Yeye alichukua mamlaka yote ya Mungu basi? Kwa kuwa mamlaka yote Mbinguni na duniani pia yako—yako ndani Yake sasa. "Mamlaka yote Mbinguni na duniani pia nimepewa Mimi." Mungu yuko wapi pamoja na mamlaka Yake? Sasa, Yesu angeweza kusema uongo? Yeye asingeweza kusema uongo. Iwapo Yeye alisema uongo, basi tuko wapi?

65 Sasa kumbukeni, wekeni. . .liwekeni hili niani mwenu, kwamba, Kanisa la Mungu aliye hai, sio dhehebu, Kanisa la Mungu aliye hai limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho. Sasa, mnapata hilo katika Mathayo Mtakatifu 17, ama, ni Mathayo Mtakatifu 16, ambapo Yeye alisema—Yeye alisema "Watu husema Mimi ni nani?"

Akasema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai," kasema Petro.

66 Yeye akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona. Mwili na damu (seminari, mtu mwingine) kamwe hakukufunulia hili, ila Baba Yangu aliye Mbinguni. Wewe ni Petro. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu."

67 Sasa, mnaona, Katoliki inasema, "juu ya Petro"; kama hiyo ni kweli, basi, yeye alirudi nyuma. Vema, Protestanti ilisema, "juu ya Yesu." Lakini sio kuwa tofauti, lakini kulinyosha jambo hili: si juu ya Yesu wala juu ya Petro, bali juu ya ufunuo wa

kiroho: "Mwili na damu havijakufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili."

68 Ndipo katika Neno lililoandikwa kwa mifano na kila kitu kingine linaweza tu kufunuliwa, na kile tu ukweli utajulikana kwacho, ni ufunuo wa kiroho. Na endapo ufunuo wako haulifunganishi pamoja, basi ufunuo wako ni wa uongo. Unaona? Halina budi kupatana.

69 Kama vile ikiwa ulikuwa unaweka mchezo-fumbo pamoja, wala hukuwa na kitu chochote hapa kando cha ku—kuangalia ilikuwa ni nini. . .ungechanganya mandhari yote. Ungesema, "Vema, ninaamini *hiki* kinaingia hapa, ninaamini *hiki* kinaingia pale." Hiyo ni akili ya binadamu. Muda si muda wajua, mandhari yako ingekuwa mbaya: itakuwa ni ng'ombe akila nyasi juu ya mti. Unaona? Kwa hiyo i—isingefanya kazi. Unaona? Lakini kama utaninii. . .laiti ungekuwa na kitu hapa cha kutumia, kutumia! "Vema, sasa," unasema, "loo, Mungu alinifunulia jambo fulani." Kama si kulingana na Neno hili, na linalifunganisha Neno pamoja, basi ufunuo wako ni wa uongo.

70 Katika Agano la Kale, kama nabii alitabiri, kama mwotaji aliota ndoto, haidhuru ilionekana halisi jinsi gani, kwanza, kabla kanisa kamwe halijaikubali, ilibidi ithibitishwe na Urimu Thumimu. Mnajua hiyo, ile naivera ya Haruni ambamo nuru ziliakisi. Sasa, wakati ukuhani huo ulipokwisha, Urimu Thumimu iliondoka nao. Bali tuna Urimu Thumimu mpya; hiyo ni Neno la Mungu.

71 Na endapo ufunuo wako haufungamani, nawe useme, "Mungu alinifunulia ya kwamba ninapaswa kubatizwa, jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," Kama hilo halifungamani na Neno, tangu Mwanzo hadi Ufunuo, na kulifunganisha pamoja, basi ufunuo wako ni wa uongo.

72 Unasema, "Mungu alinifunulia ninapaswa kubatizwa katika Jina la Yesu." Kama halifungamani na Neno, basi Urimu Thumimu hailiungi mkono. Haidhuru linaonekana halisi jinsi gani, Hili ndilo Neno la kweli. Hili ndilo Urimu Thumimu ya Mungu.

73 Sasa, "Naye Yesu. . ." Tena ninanukuu, ninarudia: "Naye Yesu akaja akasema nao (kifungu cha 18), akisema, Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu: Mkiwafundisha kuyashika mambo yote niliyowaagiza: tazama, niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari. Amina."

74 Sasa, ninataka kuwaulizeni jambo fulani, sasa ninii tu. . . Sasa, hiyo ni Mathayo 28:19, lile Andiko mnaloniomba niwaelezee, lile tunaloliangalia hapa asubuhi ya leo. Sasa, hebu tulisome hilo kwa makini, msininii tu—msilipitie mbio.

Lisomeni kwa makini. Sasa, angalieni kwa makini. "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, na la Mwana . . . " Sasa, si—si, "katika jina la Baba, katika jina la Mwana, katika jina la Roho Mtakatifu." Hivyo ndivyo watu wanavyobatiza—wanabatiza hivyo. Hilo hata si la Kimaandiko. Mnaona, sivyo, "katika jina la Baba, jina la Mwana, katika jina la Roho Mtakatifu." Hilo ni kosa. Hilo si la Kimaandiko. Wala si, "majina ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Ni, "katika Jina," j-i-n-a, umoja; Jina. Angalieni, wakati nyote mkiangalia, "katika Jina." Vema.

75 Sasa, sasa, kama kuna mahali popote ambapo hamwelewi . . . Ninamngojea Dada Sewell pale alipate. Unalo hapo? Mathayo 28:19, kifungu cha 19. Sasa, Dada Sewell, ninaamini wewe ndiwe uliyekuwa ukiliuliza kwa nguvu sana kuliko wote. Sasa, hivi hilo linasema, "Katika majina ya Baba, Mwana . . . "? Linasema, "Katika jina la Baba, katika jina la Mwana . . . "? La. "Katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu." Sio katika jina, kuweka *jina* mbele ya kila mmoja, bali tu katika Jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu. Sasa, sasa tunatambua, basi, hapana budi pawe na Jina moja pale, maana lilisema Jina moja.

76 Vema, ninataka kuwaulizeni, ni gani kati ya hayo majina inatupasa kubatizia, basi? Sasa, je, "baba" ni jina? La, kwa hiyo tusingeweza kubatiza "katika jina la Baba," maana "baba" si jina, sivyo?

77 Vema, "katika jina la Mwana," basi, tungesema. Hivi "mwana" ni jina? Mimi ni mwana, wewe ni mwana, yeye ni mwana, sawa? "Mwana" sio jina, sivyo?

78 Vema, "Roho Mtakatifu" basi; "katika jina la Roho Mtakatifu." Vema, hapa . . . Vema, ninii . . . Hebu tuseme, "Ro- . . . katika jina la Roho Mtakatifu." Hilo "Roho Mtakatifu," ni jina? La; hivyo ndivyo Yeye alivyo. Sisi sote ni wanadamu. Hivyo ndivyo alivyo; Huyo ni Roho Mtakatifu. Bali "Roho Mtakatifu" si jina; hivyo ndivyo Yeye alivyo. Sisi sote ni wanadamu, bali hilo silo majina yetu. Mnaona? La. Ni . . . kunazo sifa tatu, basi, sivyo?

79 Vema, basi, tuna kitu cha namna gani hapa, basi? Yeye— Yeye alisema, "Mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Vema, kama "Baba" si jina, na "Mwana" si jina, na "Roho Mtakatifu" si jina, hayo si majina. Kwa hiyo usingelitumia hilo kama jina, maana hakuna jina kwake hata kidogo kwanza. Sasa kama . . . Mnaelewa hilo? Hayo si majina. Hayo ni . . .

80 Kama vile tu mimi . . . Wananiita "Kasisi." Wengine wananiita nabii. Wengine wananiita mhubiri. Vema, sasa . . . Naam, mimi ni baba, mimi ni mwana, mimi ni mwanadamu; bali jina langu ni William Branham. Lakini—lakini kasisi, nabii, ama, kasisi, mzee, na mhudumu, hizo ni sifa zangu. Vema,

hizo ni za wengine wengi pia. Kama vile nafsi, mwili, na roho, hizo ni zangu, pia. Bali ni zake mwanamume, mwanamume, mwanamke, mwanamke, na wote. Mnaona? Yote ni mamoja. Mnaona, ni sifa bali hilo silo jina langu. Hilo si jina lako. Nafsi, mwili, na roho silo jina lako. Hivyo sivyo . . . hivyo ndivyo ulivyo wewe, bali si jina lako.

81 Vema, wewe ni mwanamke. Wewe ni mama. Wewe ni mke, binti. Naam, mambo hayo yote, hayo, hivyo—hivyo ndivyo tu ulivyo wewe. Na unasema wewe . . . Sikuzote nimekuita "Daktari." Ulikuwa mwuguzi. Tuseme wewe ni daktari. Vema, wewe ni mama, pia, bali hilo silo jina lako. Kama ningaliandika tu "daktari," kunao madaktari wengi. Kama ningaliandika "mwuguzi," kunao wauguzi wengi. Unaona? Bali hilo bado si jina lako. Kwa hiyo wakati mtu yeyote anaposema walibatizwa katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kama wangaliwazia tu, hata si la kiakili . . . Si—hata si—hata si sawa kiakili: jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

82 Ni kama tu Wakatoliki wasemavyo, "Uwana wa milele," Uwana wa Milele wa Kristo. Neno hilo linawezaje kuleta maana? Anawezaje kuwa wa Milele na awe ni Mwana? *Mwana*: "aliyezaliwa na." Milele haikuwa na mwanzo wala mwisho.

83 Kama wakisema kuna kuzimu ya Milele, Biblia ilisema kuzimu iliumbwa, basi inawezaje kuwa ni ya Milele? Hakuna kuzimu ya Milele; kuzimu iliumbwa kwa ajili ya ibilisi na malaika wake; si kuzimu ya Milele. Kila kitu kinachoanza, huisha. Huenda kuzimu ikawaka moto miaka bilioni mia moja, bali haina budi kuwa na mwisho, kwa sababu kila kitu kinachoanza, huisha.

84 Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kufa, kwa sababu sisi ni sehemu ya Mungu, uzao Wake, wana na binti. Tunao Uzima wa Milele, Uzima wa Mungu. Kamwe haukuanza, kamwe hautaisha. Mnaona?

85 Sasa, hili ni kali sana. Kama hamlielewi na ninahofia nitawaweka kwenye tawi moja hapa nje mahali fulani, kama vile nilivyokuwa nikizungumza na makasisi. Sasa, kama hamwelewi, niambieni, maana kwa kawaida unazungumza na makasisi namna hii. Mnaona? Lakini, mnaona ninyi wanawake, mliniuliza tu, nanyi ni marafiki zangu. [Hao dada wanajibu—Mh.]

86 Vema sasa, ninajaribu . . . Ninyi—ninyi nyote mna elimu, nanyi—nanyi nyote ni werevu. Na mimi—mimi siwataki mlichukue hili ati "kwa sababu Ndugu Branham alisema hivyo." Sasa, mimi ni mwanadamu. Naam, ninawatakeni mlichukue Neno. Na iwapo mnaweza kumpata mtu fulani atakayelidunisha Neno hilo, ninyi waleteni kwangu; kama mnaweza kumpata mtu yeyote anayesema kuna kuhitilafiana katika Neno la Mungu, mleteni kwangu. Ni . . . ha—ha—haitawezekana kabisa.

Ha—haitawezekana, hakuna haja ya kujaribu, maana hakuna, mnaona.

87 Sasa, mtu yeyote angewezaje kubatizwa...? Ninataka kuwaulizeni ninyi kina mama jambo fulani sasa hivi, ama, nanyi wanaume: Mtu yeyote angewezaje kubatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu? Ungewezaje kubatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu? Hivi huoni asili yake? Hakuna kitu kama jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hizo—hizo—hizo ni—hizo ni sifa. Mnaona? "Yungiyungi..." Mbona usiseme tu "Yungiyungi ya Bondeni, Ua la Uwandani, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega"? Ingekuwa ni sawa. Ama ungebatizwa vile vile, ukisema, "Nakubatiza kwa jina la Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho." Ingekuwa ni vile vile, ni sifa. "Ninakubatiza katika jina la Yungiyungi la Bondeni, Nyota ya Asubuhi, na Ua la Uwandani." Itakuwa ni vile vile tu, ni sifa. Lakini tunajua ni la Nani, lakini kuna...kunaweza kuwako na nyota nyingi za asubuhi, na mayungiyungi ya mabondeni, na ua la Uwandani. Mnaona? Kwa hiyo, sio...Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, kuna—kuna...hilo, ama, mwanadamu, nafsi, mwili, na roho, ama chochote cha zaidi unachotaka kulifanya.

88 Sasa, sasa kuna kasoro fulani hapa mahali fulani, sivyo? Sasa mnaona ya kwamba kuna kasoro fulani hapa. Hatuwezi kulielewa, basi, hebu tuseme. Sasa, "Basi enendeni ulimwenguni mwote, mkawafundishe mataifa yote."

89 Sasa, ninyi ni kusanyiko dogo zuri, na mimi—mimi nataka kulishindilia hili kusudi mpate ufahamu mzuri. Mnaona? Sababu sijui, wengi wa ndugu zangu huenda wakaisikia kanda hii.

90 Kamwe simwondolei ukristo mwanamume au mtu yeyote kwa ajili ya mawazo yao ya Maandiko. Ninaliweka msingi juu ya: kama wameokoka, wanamtumainia Yesu Kristo, kama ni Mkatoliki, Mprotestanti, Myahudi, ama wowote walio, umeokoka kwa sababu umezaliwa na Kristo.

91 Lakini mmeniuliza swali, "Ni kwa nini, Ndugu Branham ungebatiza katika Jina la Yesu Kristo?" Vema. "Pia ni kwa nini ungepuuza Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?" Hilo ndilo swali lenu. Na kama ndugu yenu, na kama mtumishi wa Kristo, ninawajibika kuwajibu, vema.

92 Sasa, kwa hiyo wakati unapopata hapa nje, kufanya ukinzani huu, sasa, siku kumi tu baada ya hili, baada ya Yesu kusema hili, Petro alikuwa na zile funguo za Ufalme, Mathayo 16, upate kujua, "Wewe ni Petro, na juu ya mwamba huu, kujenga Kanisa Langu," kadhalika. "Nami nakupa...Nasema ya kwamba wewe ni Petro, nami nakupa wewe funguo za Ufalme: lolote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni: unalofungua duniani, nitalifungua Mbinguni."

93 Sasa, mtu yule yule aliyekuwa na zile funguo, aligeuka moja kwa moja siku kumi baada ya Yesu kusema jambo hili, na kusema, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu." Mliwahi kusimama na kuwazia kwamba Yesu angempa mtu ambaye angechanganyikiwa kiasi hicho, funguo za Ufalme, ambaye angegeuka na kufanya vinginevyo, yale Yeye aliyosema yafanywe? Mungu wa Mbinguni aliyedhihirishwa katika mwili, naye angempa funguo mtu ambaye angefanya kosa kama hilo? Jambo la kwanza kabisa lililotoka ndani yake lingefanya kitu kama hicho? La. Kitu gani? Vema, sasa, sasa ninii tu. . . Sasa, sasa angalieni. Asingeweza kufanya hivyo.

94 Lakini ni kwa nini akazikabidhi hizo funguo kwa Petro, basi? Yeye alilinukuu tu waziwazi: "Petro, hukujifunza hili kutoka kwa kanisa fulani wala seminari fulani, bali ulikuwa ni ufunuo ambao ulitoka Mbinguni, na juu ya ufunuo uu huu kutoka Mbinguni, kulinyosha Neno la Mungu, nitalijenga Kanisa Langu." Yeye alimjua Petro: yeye hakujua—hakujua hisabati. Petro hakujua aljebra, labda, au wala hakujua jiometri, ama—ama. . . Nafikiri lilisema ya kwamba yeye alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa, kulingana na Matendo mlango wa 4, ama Matendo mlango wa 3, naamini. Kasema, "Wakitambua kwamba walikuwa wasio na elimu wala maarifa," yeye pamoja na Yohana, walimponya mtu kwenye lango lililoitwa Zuri, "bali wakatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu."

95 Kwa hiyo unaona, Yeye hakutegemea maarifa yake ya seminari ili aweze kumfunulia hili. Loo! Sio juu ya ujuzi wake wa seminari, maana hakuwa na wowote. Angali hana hata wa leo. Bali Yeye humfunulia, mnaona, yule aliyekuwa na ufunuo wake. Kwa hiyo, Yeye angeweza kuuaminishia Petro. Huenda asingaliweza, kuuaminishia Mathayo, ama Yohana, ama hao wengine. Lakini Petro alikuwa na ufunuo.

96 Kwa hiyo basi, Petro anageuka na kusema, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo," mnaona, "kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Ahadi hiyo ni kwa ajili yenu." Yule mtu aliyekuwa na funguo zilizoufungua Ufalme kwa mara ya kwanza, aliugeuza na kufanya vinginevyo, yale Yesu alisema yasifanywe. Sasa, ni kwamba ama alikosea, alifanya kosa, hakulifuata Neno la Bwana wetu, au labda, yeye alikuwa na ufunuo wa ile kweli ambao hao wengine. . . ambao—ambao ulipita ule yeyote wa hao wengine alikuwa nao.

97 Sasa, hebu tusimame tu kabla hatujarudi nyuma, kwa dakika moja tu. Kama ungekuwa ni kosa, kwa nini Mungu akautambua basi, na kuwaamuru hao wengine wote, kote katika Biblia, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo? Na kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na kila

mtu kufikia kule kuundwa kwa dhehebu la kanisa Katoliki, alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Katika Baraza la Nikea, walianzisha ubatizo huu wa Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, wakifanya Mungu wa utatu kutoka kwa Mungu mmoja wa kweli, wapate kuingiza u—utatu wao.

98 Na kwa kuwa Mungu hapo mwanzo alijua ya kwamba mwanadamu angeanguka, hivyo basi Yeye alimweka kwenye uhuru wa kujichagulia, akijua, kwa sababu angeweza kuonyesha sifa Zake kuwa Baba, kuwa Mwana, kuwa Mponyaji, kuwa Mwokozi. Yeye angewezaje kuokoa, isipokuwa kitu fulani, kipotee? Na ndani ya Mungu mlikuwamo na sifa, kabla hata hapajakuwapo na Malaika wala molekuli wala chochote, Mungu alikuwa peke Yake, pekee; ila Yeye hakuwa ni Mungu, maana hapo. . .*mungu* ni "kitu cha kuabudiwa," hapakuwapo na kitu cha Yeye kuabudu. . .kitu cha kumwabudu Yeye. Bali sifa Zake zilionyesha kitu fulani na kuumba Malaika. Ndipo akawa Mungu. Kisha akamwumba mwanadamu; akampa uhuru wa kujichagulia. Akaanguka. Basi alipoanguka, Yeye akawa ni Mwokozi. Katika kule kuanguka alishikwa na maradhi, kwa hiyo Yeye anakuwa Mponya. Mnaona? Inaonyesha sifa za Mungu. Mnaona ninalomaanisha?

99 Sasa, Yeye pia alijua ilibidi pawe na watu waliopotea na watu waliookoka. Ilibidi pawe na ubatizo wa uongo na. . .Kwa hiyo Yeye anauweka hapa, tena, mti wa maarifa: huu hapa mmoja, Matendo 2:38; mmoja, Mathayo 28:19.

100 Kwa hiyo, ilifunuliwaje kwa Habili? "Habili, kwa imani, alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi." Hakuwa na Biblia ya kutumia, kwa hiyo hapana shaka ulikuwa ni ufunuo kwa Habili. Hao hapo wavulana wote wawili. Iwapo Mungu anahitaji tu ibada, basi Mungu alikuwa asiye haki kumhukumu Kaini. Kaini alitengeneza madhabahu, akajenga kanisa, akaabudu, kisha akatoa dhabihu. Kila tendo la kidini ambalo Habili alifanya, Kaini alilifanya. Hiyo ni kweli? Lakini Habili, kwa ufunuo, alimtolea Mungu (Ni ufunuo; unatembea kwa imani.) dhabihu iliyo bora zaidi. Habili alijuaje jambo hilo, kwamba halikuwa ni tunda la kondeni, ambalo Kaini alitoa? Damu ndiyo iliyowatoa kwenye ile bustani. Uhai haukuwamo ndani ya tunda. Damu ilileta uhai. Ilifunuliwa kwake, ufunuo.

Huu hapa msingi ule ule Yeye anaotuweka juu yake ambao aliwawekea hao huko nyuma: ufunuo. Sasa, hapawezi pakawa na ukinzani.

101 Sasa, ninyi nyote sikuzote hamkuwa ni Wakristo. Mlizaliwa wenye dhambi. Nawazia kama msichana mdogo. . .Sininii—sijui kama mlifanya hivyo ama la, lakini nitachukua sisi sote chumbani, kufanya kielelezo hapa sasa, ili mweze kuelewa. Mlipokuwa wasichana wadogo, tuseme mlisoma *Magazeti ya Hadithi za Mapenzi*. Karibu wasichana wote wadogo hufanya

hivyo. Gazeti la aina yoyote; si lazima liwe ni *Hadithi ya Mapenzi*, hadithi yoyote. Mnaona? Vema. Ingewezekana... haikuwa moja ya hadithi hizi mamboleo za vibanda vya kuuzia vitabu, bali hadithi yoyote, hata kama ilikuwa ni *Romeo na Julieti*. Mnaona? Mbona u—u—u—ulisoma ha—hadithi ya mapenzi. Na endapo... Ninawaonyesha njia hii sasa, ili mweze kulishika katika mfano.

102 Kama uliokota kitabu cha hadithi, na kukisoma, nacho kilisema, "Yohana na Mariamu wakaishi kwa furaha tangu hapo na kuendelea," vema, unaanza kushangaa Yohana na Mariamu ni nani. Yohana na Mariamu ni nani? Vema, ulisoma tu maneno ya mwisho kwenye hicho kitabu; yalisema, "Basi Yohana na Mariamu wakaishi kwa furaha tangu hapo na kuendelea." Unaanza kushangaa, "Kwani Yohana ni nani, na Mariamu ni nani?" Hiyo ni kweli? Sasa, kunayo njia moja tu ya kujua Yohana na Mariamu walikuwa ni akina nani, rudi mwanzoni mwa hicho kitabu, anza kusoma. Hiyo ni kweli?

103 Vema sasa, huu ndio mlango wa mwisho wa Mathayo. Kama kitabu cha mwisho cha Mathayo, Yeye alisema, "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," na "Baba" si jina, na "Mwana" si jina, na "Roho Mtakatifu" si jina, hao ni akina nani?

104 Sasa, hebu tulichukue asubuhi ya leo juu ya msingi ule ule ambao tungechukua kwa Yohana na Mariamu. Hebu turudi mwanzoni mwa Mathayo tupate kujua. Fungueni mlango wa kwanza wa Mathayo, basi, vema. Tuone Yohana na Mariamu ni nani walioishi kwa furaha tangu hapo na kuendelea.

Tuna muda gani zaidi? Loo, vema, vema.

105 Sasa, sasa ninataka kuwaulizeni ninyi dada jambo fulani, mnaponiangalia, ninyi ndugu. Baba ya Yesu Kristo alikuwa ni nani? Alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli? Je, Mungu alikuwa ndiye Baba Yake? Vema, bwana; Mungu ndiye Baba Yake, sote tunakubaliana juu ya hilo. Ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba Mungu ndiye Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo. Vema, sasa tutaona kama Biblia inasema ya kwamba Mungu ni Baba Yake.

106 Sasa, Yesu alisema, "Basi enendeni, mkafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ninaweka vijisanduku hivi vitatu vya kumbukumbu hapa nje. *Hiki* ni Baba, *hiki* ni Mwana, *hiki* ni Roho Mtakatifu. Sasa, mna—mnaweza kuona vizuri?

107 Sasa, ninataka kuninii, ninaenda tu kuenda kuwaulizeni swali kwa dakika moja, nione kama mlisikiliza niliyosema. Ni nani *huyu* hapa? [Kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu."—Mh.] Roho Mtakatifu. Ni nani *huyu* hapa? ["Baba."] Ni nani *huyu* hapa? ["Mwana."] Sasa, ni Nani *huyu*? ["Baba."] Vema, nilitaka

tu kuona kama—kama kweli mlilishika vizuri sasa. Sasa, sasa, *huyu* ni Mwana wa Mungu, hiyo ni kweli? Vema, sasa, *huyu* hapa ni nani? ["Baba."] *Huyo* ndiye Baba wa Bwana Yesu Kristo. Hiyo ni kweli? *Huyo* alikuwa ndiye Baba Yake. Ninaamini ya kwamba Yeye ni Mwana asiyeghoshiwa wa Mungu aliye hai, aliyezaliwa na bikira.

108 Mungu, Baba yetu, ambaye ndiye Roho mkuu ambaye kamwe...Yeye alikuwa...kamwe hakuwa na umbo, hata. Mnaona, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa ninii tu... Yeye alikuwepo kabla ya nyota, molekuli, ama atomu, ama chochote kingine. Yeye ni Mungu anayejaza wakati wote, anga. Yeye ni wa Milele. Ninaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu wa kweli aliye hai. Na huyo ni Mtu *huyu* papa hapa, ambaye nimemwandika kwenye kijisanduku hiki; Baba. Hiyo ni kweli? Na *huyu* ni Roho Mtakatifu, na *huyu* ni Mwana.

109 Sasa, hebu tusome Mathayo 1. Sasa, tunaanza:

> *Kitabu cha* ukoo *wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.*
>
> *Ibrahimu alimzaa Isaka;...Isaka akamzaa Yakobo;...Yakobo...Yuda na ndugu zake;*

Kinaendelea chini kikitoa ukoo. Sasa, kuokoa wakati wetu, tutashuka chini na koo zinaisha baada...na...

> *Basi vyote*...(Kuanzia kifungu cha 17.) *Kwa hiyo vizazi vyote tangu...vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vinne; ...tangu Daudi hata uhamisho* wa *Babeli ni* vizazi *kumi na vinne; na tangu uhamisho* wa *Babeli hata Kristo ni vizazi kumi na vinne.*

Sasa:

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu...mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana* (Hivi unasoma pamoja nami, Dada Sewell?) *kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa* Mungu Baba.

110 Mimi...hivi mimi...Hivi ninasoma vizuri? Loo, nilifanya kosa? Alionekana ana Mimba ya Nani? [Mtu fulani anasema, "*Roho Mtakatifu.*"—Mh.] Vema, nitasema. Sasa, Baba Yake ni Nani? Mlisema *huyu* alikuwa ndiye Baba Yake, nayo Biblia ikasema *huyu* alikuwa ndiye Baba Yake. Alionekana ana Mimba, si ya Mungu Baba. Mungu Baba hakuwa na uhusiano wowote nayo. Ilikuwa ni Mimba ya Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli?

Hebu tuone kama hilo lingali linasomeka vizuri. Labda tulifanya kosa. Kifungu cha 19:

> *Naye Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, ...asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri;*

> *Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo: maana mimba yake ni kwa uweza wa* Mungu Baba yetu.

[Mtu fulani anasema, "La, . . . *mimba yake ni ya Roho Mtakatifu.*"—Mh.] Loo! Um-hum.

111 Sasa, sasa, basi Yupi kati ya hawa ndiye Baba Yake? Sasa, kama Roho Mtakatifu ndiye Baba Yake, naye Yesu alisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake, sasa, kwani Yeye ni mtoto haramu? Angeweza kuwa? Inawezekana miungu hawa wawili kumzaa mtoto mmoja? Kama ndivyo, Yeye alikuwa mtoto haramu. *Haramu*, sasa, ni—ni neno bora zaidi, bali hilo ne- . . . neno lenyewe linamaanisha, "mtoto haramu." Vema, basi kama Yeye alizaliwa mtoto haramu, basi tuko—tuko wapi katika wokovu? Kama Mungu Baba alikuwa ndiye Baba Yake, nayo Biblia inasema Roho Mtakatifu ni Baba Yake, basi ni wapi . . . kuna kasoro tena, hiyo ni kweli? Mnaona? Ninyi—ninyi . . . Kuna kasoro mahali fulani. Sasa, tu—tutafanya nini?

112 Hivi tunamwabudu mtoto haramu, wa Miungu wawili mbalimbali? Huyo Mungu mmoja alikuwa, alisema, alikuwa Baba Yake, kisha Bi—Biblia ilisema hapa, ama, Neno la Mungu linasema ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba Yake. Naye Yesu alisema Mungu alikuwa Baba Yake, na mahali pengine katika Biblia palisema Mungu alikuwa Baba Yake, na kumwita Yeye Mwana wa Mungu, na Mungu Baba, na sasa, Mungu Roho Mtakatifu.

113 Loo, enyi maskini watu wa Utatu, mliopofushwa! Mbona, ne—neno *utatu* hata halipatikani katika Biblia, sio kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Hakuna kitu kama hicho. Sio Miungu watatu; ni ofisi tatu za Mungu mmoja. Mungu Baba katika Nguzo ya Moto, Mungu Mwana akidhihirishwa katika mwili kuiondoa dhambi, na Mungu Roho Mtakatifu ndani yetu sasa, hapa. Hakika. Hakika. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Mnaona? Si Miungu watatu; ni Mungu mmoja.

114 Sasa, sasa angalieni. Itawabidi kukubali ya kwamba Roho Mtakatifu ni Baba Yake. Hiyo ni kweli? Hivi Roho Mtakatifu ndiye Baba Yake? Biblia inasema hivyo? Vema, angalieni hapa; hebu—hebu nilisome tena. Sasa, hebu . . . [Dada mmoja anasema, " . . . ? . . . kwamba Mungu ndiye Baba Yake."—Mh.] Hiyo ni kweli. Vema, basi, kama Biblia inasema ya kwamba Roho Mtakatifu ni Baba Yake, Roho Mtakatifu na Mungu ni Mtu yule yule, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili. Hiyo ni kweli? [Dada mmoja anasema, "Utaondolea mbali huo utatu."] Huyo hapo amelipata, jambo ndilo hilo. Tayari umeruka ukaondoka sasa, mnaona. Kamwe haikuwa hivyo hapo mwanzo. Kamwe haikuwa hivyo. Mnaona jinsi—jinsi halina budi kuja kwa ufunuo? Mnaona?

115 Sasa, sasa ama Mungu alikuwa ndiye Baba Yake au hakuwa Baba Yake. Naye Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba Yake, ama hakuwa Baba Yake, ama Biblia inasema uongo. Kwa hiyo, kuufanya huo ufunuo sahihi, na kuona kama Petro alikuwa na ufunuo uo huo nilio nao kwake, sasa, mnaona: Sasa, Mungu Baba na Roho Mtakatifu ni Roho yule yule, au alikuwa na baba wawili. Asingeweza kuzaliwa na Mungu Baba, Roho mmoja, kisha Mungu Roho Mtakatifu, Roho mwingine. Basi alikuwa na kutiwa mimba mara mbili. Mnaona? Kwa hiyo asingeweza kuwa hivyo. Kweli asingeweza kuwa hivyo. Ama moja ni kweli, na hiyo nyingine ni kweli.

116 Endapo kuna Miungu watatu, nao Miungu hawa wawili, endapo kunao Miungu wawili, mmoja, Mungu Baba, na mmoja, Mungu Roho Mtakatifu, ni yupi kati yao kweli alikuwa ni Baba Yake, basi? Swali? [Dada mmoja anasema, "Tutachukua, 'Roho Mtakatifu na Mungu ni mmoja.'"—Mh.] Sasa umelipata. Haya basi. Vema, sasa huyo ni mmoja. Vema, sasa hebu tuendelee kusoma.

Sasa tutatafuta kujua kwamba Mathayo 28:19 ni kitu gani.

Sasa, hebu nisome hiki tena sasa, kifungu cha 18:

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo...kulikuwa hivi: Mariamu...mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*

Vema.

> *Naye Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, ...*asitake *kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri;*

> *Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu...kumchukua Mariamu mkeo: kwa maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*

Vema, tunawafanya wawili, basi, hawana budi kuwa ni mmoja.

Vema.

> *Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake...* (Ati nini? Huyo ni Mtu huyu, Yesu, vema.) *utamwita jina lake YESU: maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*

> *Haya yote...yamekuwa, ili litimie neno lilonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema,*

> *Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli...* (Hiyo ni kweli?) *yaani...Mungu pamoja nasi.*

117 Sasa, Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni lipi? [Dada mmoja anasema, “Mungu.”—Mh.] La, *mungu* ni “kitu cha kuabudiwa,” sivyo? Yeye alisema nini? Ataitwa Jina Lake... [“Yesu, ama Imanueli.”] Hiyo ni kweli. [“Yesu.”] Jina Lake lilikuwa ni nani? [“Imanueli.”] *Imanueli* ni tafsiri ya, “Mungu pamoja nasi,” mnaona. Hilo linamaanisha tu, “Mungu pamoja nasi.” Mnaona? Hilo halimaanishi kusema...kungekuwako na namna yoyote ya mungu pamoja nasi, mnaona. Lakini hili likifasiriwa...Lakini Jina la Mungu huyu pamoja nasi ni lipi? [“Yesu.”] Ataitwa Jina Lake [“Yesu.”] Yesu.

118 Basi Petro aliposema...wakati Mathayo aliposema mkawabatize katika...Sasa nini...Mariamu na Yohana ni akina nani, walioishi kwa furaha tangu hapo na kuendelea? Mnaona? Mnaona kwamba ni nani? Wakati Petro alipogeuka na kusema, “Mkabatizwe katika Jina la...Tubuni mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo,” vema, alifanya vile hasa Mathayo... Kama alisema, “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” hata lisingekuwa sawa kiakili.

119 Sasa, “Kwa nini unabatiza, Ndugu Branham, katika Jina la...la Yesu Kristo?” Sasa, hebu tufungue hapa sasa nasi tutaangalia tu. Sasa, ni nani aliyekuwa na zile funguo za Ufalme? [Mtu fulani anasema, “Petro.”—Mh.] Ni nani aliyenena kwenye Siku ya Pentekoste, sasa, na kusema, “Tubuni mkabatizwe kila mmoja katika Jina la Yesu Kristo?” [Mtu fulani anasema, “Huyo angekuwa ni Petro, sivyo?”] Vema, basi funguo zilifunga, “Utakachofunga duniani, nitakifunga Mbinguni.” Hiyo ni kweli? “Utakachofungua duniani, nitakifungua Mbinguni.” Hiyo ni kweli?

120 Sasa, ni makabila mangapi yaliyopo duniani? Matatu: Hamu, Shemu na Yafe-...watu wa Shemu na Yafethi. Sasa, hayo ni Myahudi, Mmataifa na Msamaria, mnaona. Vema, wote walitokana na hao wana watatu, kama ninii...Vema, Mungu anisamehe, kusema, “*Kama* Biblia ni ya kweli.” Hakika hiyo ilikuwa... Ulimwengu wote uliangamizwa ila hao—hao wavulana watatu. Hapo—hapo hasa ndipo vizazi vyetu vilipotokea.

121 Sasa, mamajusi watatu walikuja kumwona Yesu. Falaki inasema ya kwamba wao, wakizifuata nyota tatu mbalimbali, nazo hizi nyota tatu ziliunganika na kufanya nyota moja. Mnaona? Nazo hizo tatu ni moja, daima. Mnaona?

122 Sasa, hizo sifa tatu za Mungu zinamfanya Mungu mmoja. Sio Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Sio Miungu watatu. Yesu...Filipo aliuliza swali hilo, “Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.” Yohana 14.

Yeye akasema, “Nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, Filipo, hunitambui?” Akasema, “Ukiisha kuniona Mimi, umemwona Baba.”

123 Sasa, nilikuwa nikielezea hili kwa baadhi ya wanawake siku moja, ndipo mwanamke ali-. . .vema, kasema, "Ngoja kidogo tu, Ndugu Branham." Kasema, "Wao ni mmoja. Hiyo ni kweli." Kasema, "Vivyo hivyo wewe na mke wako, mmoja."

Nikasema, "Ila Wao ni aina nyingine ya Umoja."

Naye akasema. . . Nikasema. . . "Loo," akasema, "la, Wao ni kama wewe na mke wako, mmoja."

Nikasema, "Loo, la, unaona," nikasema, "unaniona mimi?"

Akasema, "Ndiyo."

Nikasema, "Unamwona mke wangu?"

Akasema, "La, hata simjui mimi."

124 Nikasema, "Basi Yesu alisema, 'Ukiisha kuniona Mimi, umemwona Baba.'" Kwa hiyo nikasema, "Wao, kwa hiyo Wao—Wao ni Umoja wa aina nyingine." Mnaona? Nikasema, "Unaniona mimi, bali humwoni mke wangu. Bali unapomwona Yesu, unamwona Mungu." Yeye alimdhihirisha Mungu. Yeye alikuwa ni Mwana aliyezaliwa na bikira. Naye Mungu Baba, ambaye ni Roho, aliishi ndani Yake.

125 Sasa, wa Utatu wengi—wengi wanajaribu kusema. . . Nilikuwa nikilijadili sio muda mrefu uliopita. Nikakuta kwamba haifai kitu, kwa sababu hakuna mtu anayeweza kuja kwa Mungu isipokuwa Mungu alimjua tangu zamani na kumwita kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu," kasema Yesu. Mnaona?

126 Ndipo mtu huyu akajaribu kusema. . . Yeye alikuwa wa—wa Utatu, kupindukia, naye akasimama mbele ya hilo darasa na kusema, "Rafiki zangu wapendwa," kasema, "Ndugu Branham ni mmoja wa jamaa walio wazuri sana." Unaona, unaona mara moja, nilijua kulikuwako na jambo fulani.

Yesu alisema, "Enyi wanafiki, mnawezaje kusema mambo mazuri? kwa kuwa kinywa hunena yale yaujazayo moyo." Mnaona?

127 Na kwa hiyo, akijaribu tu kupata kibali kwa hao watu, yeye alisema. . .Huyu alikuwa ni mtu wa Church of Christ, na, linalojiita Church of Christ. Bila shaka wanapinga mafundisho yote ya kweli ya Biblia, karibu yote, wala usingeweza kuwarejesha. . .Sikusudii kusema lolote dhidi ya hao watu mle ndani, bali hao wahudumu ni, kama—kama mtaruhusu tamshi hili, "Ni kama bundi wa Muairishi: mahangaiko chungu nzima na manyoya, wala hakuna bundi." Kwa hivyo hivyo ni karibu jinsi ilivyo, mnaona, ninii tu. . . ha—hawana chochote cha kusimamia, kwa hiyo, Farisayo mamboleo.

128 Sasa, yeye alisema, "Lakini Ndugu Branham amekuwa kama ninii, katika majadiliano haya," kasema, "anagaagaa kutoka kwenye kila kitu, kama mdudu katika limau." Lakini kasema,

"Ningemtaka agaagae atoke kwenye hili." Na bila shaka wajadili wote hushikilia wazo lililo muhimu sana mpaka sehemu yake ya mwisho. Kwa hiyo basi akasema, "Kwenye ule ubatizo katika Mathayo 3, yale madhihirisho ya watu watatu, kabisa watu watatu mbalimbali: Mwana akisimama ufukoni; Roho Mtakatifu, kama hua, katikati yao; Mungu Baba, akinena kutoka Mbinguni."

Nikasema, "Bwana, hilo ndilo neno lako la kumalizia?"

Akasema, "Ninataka kukusikia ukigaagaa utoke kwenye hilo."

129 Nikasema, "Bwana, wewe gaagaa urudi na kuyasoma Maandiko, jinsi yalivyoandikwa." Nikasema, "Hilo ndilo jambo pekee; unawasomea tu watu Maandiko vibaya." Nikasema, "Hilo ni jembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Mbona, unaninii tu . . . una—una—unaliweka vibaya, ndugu. Unawasomea watu vibaya." Kisha nikasema, "Sasa, angalieni hapa vile huyu ndugu anavyosema."

130 Sasa, nitalichukua namna hii, kama *hawa* nilio nao: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Sasa, *hiki* hapa kingekuwa Roho Mtakatifu, *kile* kimeandikwa, "Mwana," *hiki* kimeandikwa, "Baba." Sasa, angalieni jinsi wanavyoyasoma hayo: "Yesu alipobatizwa . . . alitoka mara moja majini: tazama, mbingu zikamfungukia, akamwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka, na Sauti kutoka Mbinguni, ikisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.'" Nikasema, "Mnaona, maelezo matatu mazuri: Mwana akiwa ardhini, Roho Mtakatifu kama hua kati yao, na Baba kutoka Mbinguni akinena." Mnaona jinsi ibilisi anavyoweza kusimama pale na kumdanganya mtu, iwapo huna ufunuo wa Mungu, Mungu asipoturehemu? Inatupasa kushukuru.

131 Yeye alilifanya hilo liseme jambo fulani halikusema, kama tu Mathayo 28:19, kuyafanya yaseme jambo fulani hayakusema. Kamwe Yeye hakusema, "Mkawabatize . . . " Kamwe hakusema, "Mkawabatize katika jina la Baba, katika jina la Mwana, jina la Roho Mtakatifu." Kasema, "Mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," ambalo ni Yesu Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

132 Sasa, hebu tuchukue maelezo haya. Sasa, hebu tuone. Mnayaandika Maandiko, Mathayo 3 pale, vifungu vitatu ama vinne vya mwisho. Sasa . . . [Mmoja wa wale kina mama ananena—Mh.] Vema, hilo ni sawa, atalipata nanyi mnaweza kulisoma mtakapofika . . . Ninawapeni Maandiko ili mweze kuyasoma peke yenu. Sasa, angalieni, tazameni.

133 Sasa, wao wanasema huyo alikuwa ni Mwana amesimama ufukoni; huyu ni Mungu Roho Mtakatifu, kama hua, katikati

yao; naye Mungu Baba alikuwa akizungumza kutoka Mbinguni. Sasa, inaonekana kana kwamba hilo lingefanya sauti tatu mbalimbali hasa kutoka mahali patatu mbalimbali. Sasa, angalieni. Sasa, Yesu alipobatizwa. . .

134 Sasa, tunatambua ya kwamba *mbingu* zilikuwa. . . zinamaanisha "juu, anga," chochote kile, mbinguni. Sasa, "Yesu alipobatizwa, mara alipanda kutoka majini: na, tazama, mbingu zikamfunukia, naye akaona Roho wa Mungu. . ." Nilidhani walisema Mungu alikuwa huko juu Mbinguni akinena. "Roho wa Mungu kama hua. . . " Huyo hua alikuwa ni Mungu. Mnaona? Ndio kwanza tulipitie hapa. Roho Mtakatifu na Mungu ni Mtu yule yule. Mnaona? Ni sifa tu kwake. Mnaona? Naye akamwona Roho wa Mungu. Sio Mungu mwingine huko juu Mbinguni akinena, bali Roho wa Mungu alikuwa katika mfano wa hua. Huyo alikuwa—huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu naye alikuwa ni Mungu, jambo lile lile, mnaona?

135 Roho wa Mungu, kama hua, alishuka, na Sauti kutoka Mbinguni, ambayo ilikuwa juu Yake, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Kweli, tafsiri sahihi (Wameweka kitenzi kabla ya kielezi, kama wageni wote.) ni, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Ama, "Ambaye ninapendezwa kukaa." "Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Huyo alikuwa ni Mungu akija ndani ya Yesu, na ndani Yake ulikuwa Utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Basi huyo hapo Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wako: katika Jina la Yesu Kristo.

136 Hakika. Mnalipata? Hakuna—hakuna mahali katika Biblia, panapozungumza juu ya watatu, kwamba ni miungu watatu. Hakuna kitu kama hicho. Ni ukafiri kabisa. Ulitoka kwa upagani. [Dada mmoja anasema, "Vema, hilo linaondolea mbali utatu huo."—Mh.] Naam. Vema, hakika, ni. . .kuna. . . wao. . .ni kama tu—halina mwisho kadiri kuzimu kulivyo. Mnaona? Hakuna kitu kama hicho. [Dada mmoja anasema, "Billy Graham anahitaji hilo."] Unasema nini? ["Billy Graham anahitaji hilo."] Vema, asingeninii. . .?. . .hilo. [Dada mmoja anasema, "Nililihitaji pia. . .?. . . "]

137 Angalieni, sikilizeni. Linafunuliwa wale ambao Mungu anawaita na wamekusudiwa tangu zamani kwa kujua Kwake tangu zamani. "Kondoo Wangu wote wanaisikia Sauti Yangu." Mnaona? Waangalieni hao Wayahudi wamesimama pale, wa kielimu tu walivyoweza kuwa, naye Yesu akiwaonyesha Yeye alikuwa ni Masihi kwa ishara ya Kimasihi. Wakasema, "Yeye ni Beelizebuli." Wangewezaje. . .? Walipofushwa. Naam, na maskini mchungaji anayeparuza ama—ama mvua samaki huko mtoni, kasema, vema, wao walimfahamu. Mnaona? Yeye ananinii tu. . .Mungu anayo njia ya kufanya mambo na inatupasa tu

kuvumiliana na njia Yake. Mimi. . .Shukuruni tu kwamba macho yenu yangeweza kufunguliwa kuiona kweli.

138 Sasa, nitampa changamoto mtu yeyote (sio kwa ajili—sio kwa ajili ya kubishana), atakayekuja kwangu na kuketi chini na kunionyesha mimi *utatu* wakati mmoja katika Biblia, ama ambapo pana miungu watatu. Kama utanionyesha miungu watatu, nitakuonyesha tuko gizani, na wapagani, na makafiri. Kuna Mungu mmoja tu.

139 Mungu, Mungu Baba, kweli tunaamini hilo. Yeye alikuwa huko juu ya wote, juu ya mlima huu; hapo aliposhuka juu ya ule mlima kule juu, mbona, hata kama ninii. . .kama ng'ombe aliugusa huo mlima, ilibidi auawe: Mungu Baba. Lakini Yeye alitaka kurejesha ushirika pamoja na mwanadamu Wake. Yeye anajaribu kumrudisha mwanadamu huko Edeni ambako alipotelea. Mnaona?

140 Sasa, jambo lingine alilofanya, ndipo Mungu Baba akamtia uvuli bikira aliyeitwa Mariamu. Nayo himoglobini (Unajua hili, kwa kuwa muuguzi.), seli ya damu hutokana na mwanamume. Kisha mtu fulani akasema, "Tunaokolewa kwa damu ya Kiyahudi." Hakuna chembe moja ya damu ya mama katika mtoto mchanga. Mtoto mchanga hukaa katika damu ya mama, bali seli ya damu hutoka kwenye jinsia ya kiume. Kwa hiyo Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa; Yeye alikuwa ni Mungu, Damu umbaji, si kwa tamaa ya kujuana kimwili, bali Damu umbaji. Mnaona ninalomaanisha? Halafu basi, Damu ya Mungu ilituokoa, Damu isiyoghoshiwa.

141 Yeye alijiumba Mwenyewe. Ninamaanisha Yeye alibadilisha sifa Yake kutoka kwa Mungu akawa mwanadamu na kushuka chini, akazaliwa na bikira, Mariamu; naye Roho Mtakatifu (ambaye ni Mungu, Baba Yake aliyemtia uvuli) alishuka na kutandaza hema Yake na kuishi pamoja nasi katika umbo la mwanadamu. Huyo ni Mungu Mwana, Mungu yeye yule aliyekuwa Mungu Baba. "Si Mimi ninayezitenda hizi kazi. Ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu; Yeye huzitenda hizi kazi." Mnaona? [Dada mmoja anasema, "'Aliye *ndani* Yangu.'"—Mh.] Hiyo ni kweli.

142 Baba anayeishi, anayefanya maskani, anayeishi. "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake." Mathayo 3. Mnaona? "Ninayependezwa kukaa ndani Yake. Ninapendezwa sana kukaa katika Huyu." *Kukaa*, hiyo, "kukalia, kuingia ndani ya nyumba na kuishi." "Ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili," yanasema Maandiko. Hiyo ni kweli, sura inayoonekana ya Mungu asiyeonekana. Sasa, Huyo hapo. Sasa, huyo ni Mungu Baba, Mungu Mwana.

143 Na sasa, kupitia kwa kuvunjwa kwa hiyo seli ya damu. . . Wakati maskini kuhani wa kale katika Agano la Kale, chini ya ule utaratibu wa kale, mwenye dhambi alileta mwana-kondoo,

akaweka mkono wake juu ya huyo mwana-kondoo, shingo yake ikakatwa, kwa sababu alikuwa ametenda dhambi, naye mwana-kondoo huyu akafa kwa ajili ya dhambi zake. Sasa, sababu ya yeye kutoka nje, inasema Waebrania, akiwa na tamaa ile ile aliyokuwa nayo akiingia ndani (Kama alifanya uzinzi, yeye anarudi akiwa na tamaa ile ile; kama aliua, anatoka nje anarudi, tamaa ile ile, chuki.), kwa sababu wakati hiyo seli ya damu ya mwana-kondoo ilipovunjwa, seli hiyo ya damu katika huyo mwana-kondoo ilikuwa ni uhai wa mnyama, isingeweza kurudi na kuishi katika uhai wa mwanadamu, kwa sababu uhai wa mnyama hauna nafsi, bali uhai wa mwanadamu una nafsi. Mnaona?

144 Mnyama hana nafsi. Hajui mema na mabaya. Haimbidi kuvaa nguo na kuufunika uchi wake; na kusema maneno mabaya, nanyi mwajua ninalomaanisha. Mnaona? Wao—wao hawajui. Walianguka kwa sababu wako chini yetu. Mnaona? Wanadamu wako juu ya uhai wa mnyama, maana wao—wao ni mungu wa uhai wa mnyama. Hiyo ni kweli.

145 Ilikuwa, hapo mwanzo, kwa sababu Adamu aliwapa majina na alikuwa na mamlaka juu yao. Mwanzo 1:26, alikuwa na mamlaka juu ya dunia nzima. Yeye alikuwa—alifanywa katika sura ya Mungu naye alifanywa kuwa mungu m—mdogo. Yesu alisema hivyo. Kasema, "Hivi torati yenu haikusema ninyi ni miungu? Na kama waliwaita miungu hao waliojiliwa na Neno la Mungu, ambao walikuwa ni manabii, mnanihukumuje ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Mnaona, haya basi.

146 Sasa, sasa, katika hili, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu . . . Sasa, baada ya Yeye kuishi katika ile Nguzo ya Moto, kisha akashuka na kujifanyia Mwenyewe mwili, akajishushusha Mwenyewe kwenye hema ya mwili wa binadamu na kuishi mle, miongoni mwetu; Mungu akiishi. Timotheo wa Kwanza 3:16: "Bila shaka," Paulo akinena, "siri ya utauwa ni kuu: kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na . . . " Naam, Mwumba akawa Mwokozi. Katika ule wimbo mkuu ambao Booth-Clibborn aliandika: "Yule Muumba mkuu akawa Mwokozi wangu, na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake." Mnaona?

147 Sasa, angalieni. Baba, wakati huo alikuwa ni Baba, huko juu yetu kabisa. Hata usingeweza kukaribia mahali alipokuwa. Ndipo akawa Mwana, ili tuweze kumgusa, kumhisi Yeye. Alikuwa ni Mwanadamu. Kisha akautoa Uhai Wake. Ile Seli ya Damu ilivunjwa na mkuki katili wa Kirumi, wenye dhambi hapo ulipouchoma moyo Wake. Na, kweli, moyo uliovunjika ulimwua; maji Yake na Damu yakatengana. Huzuni iliivunja Seli, ya huzuni, kwa sababu ya dhambi ya jamii ya binadamu. Tulizoea kuimba maskini wimbo mdogo:

Loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
Alikuwa nao kwa ajili ya jamii iliyoanguka ya Adamu,
Akamtoa Mwanawe wa pekee apate kuteseka,
Na kutukomboa kwa neema Yake.

148 Sasa, hapo Seli ile ya Damu ilivunjwa. Sasa tunapoweka mikono yetu kwa imani juu ya huyo Mwana-Kondoo wa Mungu anayetetemeka, tunauhisi mwili Wake ukitetemeka na kutikisika kwa ajili yetu, nayo mikono yetu inalowa kwa Damu Yake, na nafsi zetu, ule Uhai uliokuwamo ndani Yake haukuwa ni mwanadamu tu, wala haukuwa ni mnyama, ulikuwa ni Mungu, kwa hiyo Uhai huo hurudi juu ya aliyetakaswa, naye anakuwa mwana ama binti, uzao wa Mungu, mnaona, Uhai wa Mungu. Nasi ni wana na binti za Mungu kupitia kuvunjika kwa ile Seli ya Damu, Yesu Kristo.

149 Sasa, ni kitu gani basi? Mungu amerudi ndani ya watu Wake, akifanya ushirika kama alivyofanya katika bustani ya Edeni. Mnaona? Haya basi, wana na bint-. . .si ni zuri hilo? Wewe, unaona? Mungu amerudi . . .

150 Sasa, sasa, tutamaliza ubatizo; kisha sina budi kuondoka. Sasa, tangu wakati huo, sasa, mara nyingine ubatizo umenenwa, Filipo alishuka na kuwahubiria Wasamaria. Matendo 8, ninaamini ndiyo, naam, Matendo 8 (7, Stefano alipigwa mawe), nafikiri ni Matendo 8, ambapo Filipo alishuka, akawahubiria Wasamaria. Nao wote, walikuwa wamebatizwa, kila mmoja wao, kwa Jina la Yesu Kristo; ila Roho Mtakatifu hakuwa amemshukia yeyote wao bado.

151 Petro alikuwa na zile funguo. Naam, ilibidi akifungulie kizazi hicho. Ndipo wakati anaposhuka, naye Roho Mtakatifu hakuwa amemshukia yeyote wao bado, hata hivyo walikuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Petro alishuka, yeye na Yohana, na kuweka, Petro akawawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

152 Sasa, ndipo wakati Petro alipokuwa juu ya dari wakati mmoja, kwa nyumba ya Simoni mtengenezaji wa ngozi, aliona ono. Kwa sababu Kornelio Mmataifa . . .Huyo hapo Myahudi, Msamaria, sasa Mmataifa. Naye Petro alikuwa juu ya dari, akilala usingizi mdogo kabla ya chakula cha kutwa, wakati wakikiandaa chakula cha kutwa, ndipo akaona shuka likitelemshwa chini. Kila namna ya vitu vichafu, wanyama watambaao kutoka ardhini walikuwa juu yake. Ndipo basi alipofanya hivyo, akasikia Sauti, ikisema, “Ondoka, Petro, uchinje ule.”

Akasema, “Hakuna kitu kichafu kilichopata kuingia kinywani mwangu.”

Kasema, "Usikiite kichafu kile ninachoita, ama, najisi na kichafu kile ninachokiita safi." Mnaona, hao walikuwa ni Wamataifa.

153 Ndipo basi wakati alipotoka kwenye hilo ono, kulikuwako na watu wawili waliosimama langoni, wakimwita akwee. Naye akasema, ama, Roho akamwambia, "Ondoka uende. Usiwazie lolote, ondoka tu uende pamoja nao." Akaenda nyumbani mwa Kornelio.

154 Akawakusanya . . . Kornelio alikuwa ni akida, naye akaita watu wake wote pamoja. Nao wote walikuwa mle ndani, naye Petro alikuwa akiwaelezea yale yaliyokuwa yametukia, akazungumza . . . Ndipo Kornelio akamwambia ya kwamba alikuwa amemwona Malaika ambaye alimwambia aende akamwite Simoni, kwa—kwa nyumba ya jamaa mmoja Simoni mtengenezaji wa ngozi. Basi Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia hao waliolisikia hilo Neno. Naye Petro akasema, "Tunaweza kuzuia maji, kwa kuwa wamempokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?" Naye akaamuru wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.

155 Sasa, Matendo 19, kama mkitaka . . . Hiyo ni Matendo 10:49 pale, dada, unaliandika, unaona, Matendo 10:49, vema, 10:47, na kuendelea hata mwisho wa huo mlango, uusome.

Na basi wanapofika sasa kwenye Matendo, Matendo 19, ubatizo unatajwa tena. Paulo . . . Sasa, sasa hiyo inamfanya kila mtu . . .

156 Sasa, wakati pekee ambapo ubatizo ulipata kufanywa ulifanywa na Yohana Mbatizaji, kwanza. Walibatizwa kule. Wao . . . Sasa, bali hawakubatizwa katika Jina la Yesu, maana hawakujua Yeye alikuwa ni Nani bado. Mnaona? Sasa, lakini sasa, wakati . . . Yesu alisema, Mathayo 28:19, "Mkawabatize, Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," na kutoa tamshi hilo kwa yule mtu ambaye Yeye alimpa zile funguo, ambaye alikuwa na ufunuo wa yale hayo yote yalihusu, amefunuliwa kutoka Mbinguni.

157 Huo ndio mnaoupokea sasa hivi, ufunuo kutoka Mbinguni kulinyosha. Utalenga shabaha kama mtadumu moja kwa moja nao. Umelengwa vema. Utapiga shabaha basi. Petro alikuwa na ono, akalilenga kikamilifu. Hili linafanya hivyo pia. Linalirudisha ndani moja kwa moja. Bunduki ikipiga mahali inapopaswa kupiga, sasa. Mnaona?

158 Sasa, basi Paulo alikuwa—alikuwa ni mtume kwa Mataifa. Hiyo ni kweli? Alikuwa ni wa Mataifa . . . Maana Mungu alimtuma kwa Mataifa. Sasa, sasa hapa, kila mtu basi alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo; kila mmoja. Wayahudi, walibatizwa katika Jina la Yesu? Matendo 2:38? Wasamaria, Matendo

8? Walibatizwa katika Jina la Yesu? Vema, Mataifa? Katika Matendo 10:49? Walibatizwa katika Jina la Yesu, sivyo?

159 Vema, sasa, kulikuwako na watu wengine waliokuwa wakikimbia huko ambao hawakubatizwa katika Jina la Yesu, ingawa wamebatizwa. “Nadhani itakuwa ni sawa basi. Kwa hiyo achaneni tu nao, maana wamebatizwa. Inaleta tofauti gani?”

“Walibatizwa na Yohana,” wakasema. Vema, hiyo—vema, hiyo, kile tunachotaka kuona sasa, tunataka kuona kama huu ni muhimu ama si muhimu. Mungu asifiwe.

160 Matendo 19, Paulo akiisha kupitia kati ya nchi za juu za Efeso, aliwapata wanafunzi fulani. Sasa, kulikuwako na maskini mhubiri mdogo wa Kibaptisti, kule juu, nalo jina lake lilikuwa Apolo, ambaye alikuwa, Apolos, hasa. Naye alikuwa mtu mwenye akili sana; sasa, Matendo mlango wa 19. Naye alikuwa—alikuwa ni mtu mwenye akili sana, naye alikuwa—alikuwa akithibitisha kwa Biblia, kama Mbaptisti halisi, ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo, kwa Biblia. Nao walikuwa na u—uamsho huko juu, uamsho mkuu.

161 Naye Paulo alikuwa amewekwa gerezani kwa ajili ya kutoa pepo, kutoka kwa mpiga ramli, na kwa hiyo . . . yeye pamoja na Sila. Basi usiku mmoja wakaingilia kuomba mle ndani na kuimba nyimbo; ndipo Bwana akashuka, akaitikisa hiyo jela sana. Kwa hiyo, basi, akiisha kukombolewa, alitoka akamchukua akida na kumbatiza pamoja na mke wake, kama tabia ya Paulo. Bila shaka walibatizwa katika Jina la Yesu, halafu basi . . . walipompeleka pamoja na familia yake nje na kuwabatiza. Ndipo basi Paulo akaenda zake.

162 Basi akaenda kwa Akila na Priska, ambao walikuwa watengeneza hema, marafiki zake, waongofu wa Kristo. Nao walikuwa wakihudhuria uamsho huu hapa juu pamoja na Wabaptisti hawa. Mlango wa 18 ndipo mngesoma hilo, mlango mmoja tu awali. Kwa hiyo basi—kwa hiyo basi Paulo akapitia nchi za juu za Efeso. Anakutana na baadhi ya wanafunzi. Walikuwa ni wanafunzi. Walikuwa ni Wabaptisti, mhubiri mzuri na kila kitu, akithibitisha kwa Biblia, Yesu alikuwa ni Kristo. Naye akawaambia, “Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

163 Jinsi wewe ndugu wa Utatu na dada, mlipenda sana kuwawekelea hilo Wabaptisti; lakini nashangaa kama nasi tunaweza kuwawekelea kitu kingine tena. Hmm. Mnapenda kusema, “Sasa, ninyi Wabaptisti, nilidhani mlisema mlimpokea Roho Mtakatifu mlipoamini. Paulo alisema, ‘Mmempokea Huyo tangu mlipoamini?’”

Nao watu hawa walikuwa ni waaminifu. Wakasema, “Hatujui kama kunaye Mmoja, Roho Mtakatifu yeyote.”

164 Sasa, kama haileti tofauti yoyote, baada ya huo, ya ubatizo, ubatizo wa maji hauleti tofauti yoyote, basi ni kwa nini mtume huyu akauliza swali hili? Kasema, "Basi, mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

165 Loo, huenda walisema hivi: "Loo, tumebatizwa," wakasema, "tumebatizwa kwa Yohana, nasi tumeridhika vizuri sana nao, mtu yule yule aliyembatiza Yesu Kristo, shimo lile lile la maji." Hakika, nadhani kama wewe—wewe ulibatizwa na Yohana papo hapo kwenye shimo lile lile la maji, alimobatiziwa Yesu, ungedhani ulikuwa ni mzuri sana, sivyo?

166 Lakini kumbuka, zile funguo zilifungwa Mbinguni. Petro alifanya hivyo kwenye Siku ya Pentekoste. Naam—naam, bwana. Naam, bwana. Mnaona? Ni siri. Imefichwa sasa. "Lolote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni." Huu hapa ufunuo. Unaweza tu kuja kupitia kwa ufunuo huu. Mnaiona ile mbegu?

167 Paulo alisema, "Lakini huo hautafaa kitu tena. Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" yeye alisema.

Kasema, "Hatujui, kama kunaye Roho Mtakatifu yeyote."

Kasema, "Basi, mlibatizwa kwa ubatizo gani?" ama vinginevyo, "mlibatizwaje?"

168 Wakasema, "Tayari tumebatizwa. Loo, naam, bwana. Naam, Bw. Mtume Paulo, tumebatizwa. Tulibatizwa na Yohana Mbatizaji, pale pale kwenye shimo lile lile la maji alimobatiziwa Yesu Kristo. Kama alikuwa ni mzuri vya kutosha kumbatiza Yesu, ama, kuba-. . .mbona yeye, jamani, nakwambia, yeye ni mzuri kutosha kwangu. Haleluya!"

Kama wangalifanya hivyo, kamwe wasingalimpata. Lakini Paulo alisema, "Je, mmempokea Huyo tangu mlipoamini?"

Kasema, "Hatujui kama kunaye Roho Mtakatifu yeyote."

Kasema, "Basi, mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

Wakasema, "Kwa Yohana."

169 Akasema, "Yohana alibatiza tu kwa toba, akisema walipaswa kumwamini Yeye ajaye, hiyo ni kusema, Yesu Kristo." Na hapo waliposikia jambo hili, walibatizwa upya katika Jina la Yesu Kristo. Hiyo inalileta kundi *hili* juu ya kundi *hili*. Nao wakaweka mikono yao juu yao, nao wakanena kwa lugha na kutabiri.

170 Sasa, nitawaambia, kwamba kila Andiko katika Biblia, kila mtu katika Biblia, alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Ninamchukua mtu yeyote, mwanahistoria yeyote, kwenye jukumu hili: kama unaweza kunionyesha chembe moja ya Andiko ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa, katika Biblia (lile kanisa jipya, hakika, hawakubatizwa katika Agano la Kale, bali katika Agano Jipya), ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa

katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, mahali pamoja ambapo *hiyo* iliwahi kutajwa juu yao, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," basi nitapatana.

171 Na kama ninyi. . .nami nitawaonyesha. . .Kama unaweza kunionyesha fungu moja la Maandiko ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, ama chembe moja ya historia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa, kufikia kuundwa ama kuwekwa utaratibu kwa kanisa Katoliki katika mwaka wa mia sita A.D. . . .325 ndivyo ilivyo, 325 A.D. miaka mia tatu na ishirini na tano baada ya wale mitume, kila mtu aliendelea kubatiza katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, ama, katika Jina la Yesu Kristo mpaka 325.

172 Halafu, wao wakaunda dhehebu. Na katika hilo dhehebu, ambalo Kanisa Katoliki ndilo mama ya madhehebu yote, Mungu kamwe hakuliundia kanisa dhehebu, bali mle ndani walibadilisha jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, kwa sababu ya wale wa Utatu. Ndipo walikuwa na kundi kubwa lililozama kabisa katika Utatu, na kundi kubwa lililozama kabisa katika Umoja, ambapo makundi yote mawili yamekosea. Mnaona? Ila hakuna. . .Na mtu yeyote ambaye amebatizwa kwa kutumia sifa hizo za Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, pasipo kujua, wanakubali kwamba wao ni Wakatoliki na wanakana yale Biblia isemayo.

173 Sasa, ndugu zangu, nanyi mnaoisikiliza kanda hii, "Mimi—na—najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua." Msilitupilie tu hili mbali, wanawake hawa, nikiwasilisha hili kwenu, bali mnaliwajibikia wenyewe kuketi chini na kulisoma na kutafuta kujua. Iwapo wewe si. . .Endapo wewe ni mtoto wa Mungu, kweli utalititilia maanani sana.

174 Neno la Bwana liliwajia manabii katika siku za kale. Sababu ya wao kuwaita "manabii," ni kwa kuwa walikuwa na tafsiri ya Neno la Kiungu, kwa sababu walitumwa kiungu, nazo ishara na maajabu yaliyowafuata yalithibitisha ya kwamba walitumwa. Mungu amesema katika Maandiko Yake, "Kukiwako na nabii miongoni mwenu, na kama akisema mambo na si ya kweli, hayatimii, basi msimwogope. Lakini kama yakitimia, basi msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye." Nalo neno lenyewe *nabii* linamaanisha "mfasiri wa Kiungu wa Neno la Kiungu." Ishara na maajabu yanayolidhihirisha Neno ni ishara kwamba lilikuja. Sasa, tunaamini ya kwamba karama ya unabii inayoyafunganisha maneno pamoja ni vivyo hivyo.

175 Sasa, si muda mrefu uliopita, na labda mtu yuyo huyo huenda akaisikiliza kanda hii siku moja, ambapo mimi, ambapo—ambapo hili lilitukia. Ilikuwa ni Ndugu Scism wa Umoja. Sasa, ninyi—ninyi. . .wengi wenu watu mnaosikiliza hii, mngesema, "Ndugu Branham ni wa Umoja." Sivyo nilivyo.

Nafikiri ninyi nyote wawili mmekosea, wa Umoja na wa Utatu pia. Sio kuwa tofauti, bali sikuzote ni katikati ya barabara.

176 Kama Isaya alivyosema, Isaya 35 ilisema, "Kutakuwako na njia kuu." Nanyi ndugu Wanazarayo, na kadhalika, mnasema, "Njia nzuri kuu ya utakatifu." Samahani; Hilo halisemi, "Njia kuu ya utakatifu."

177 Lilisema, "Kutakuwako na njia kuu na..." (*na* ni kiunganishi) "...na njia, nayo itaitwa, 'Njia ya utakatifu.'" Sio njia kuu ya utakatifu. Njia iko katikati ya barabara. Kila upande ndiko waangukao hurukia. Hapo ndipo ninyi ndugu wa Umoja mlipoenda upande mmoja, wa Utatu wakaenda upande mwingine, bali Ujumbe wa kweli uko katikati ya barabara.

178 Sasa, angalieni hapa. Kama mtaelewa sasa, ninaweka vitu vitatu huku. Sasa, ninachukua hiki kuwa yale Mathayo aliyosema, na kuwaonyesha ya kwamba watu hao wote wawili walisema jambo lile lile. Lakini mmoja, watu wa Utatu, kwa, ninachukia kusema hili, wala sitaki kulisema, bali sitaki kusema "kwa kutokujua," kama Biblia ilivyosema, bali ninamaanisha, ya kwamba, kwa kutafsiri vibaya, hamwezi kulifanya liende sawasawa, ndugu. Kamwe hamtalifanya liende sawa. Haliwezi mpaka mtakaporudi kwenye ule ufunuo, ndipo Maandiko yote yataenda sawa.

179 Sasa, angalieni hapa, dada zangu, nanyi ndugu m—mliopo: Mathayo alisema, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Sasa, kama mtaenda mchukue *Emphatic Diaglott* ya tafsiri ya Kiyunani (tafsiri asili ya Kiyunani kutoka Vatikani; inatokea kwamba ninayo moja; hakipatikani—hakipatikani sasa, nafikiri), ama tafsiri yoyote ya Kiyunani, tafsiri ya kweli ya Matendo 2:38: Petro alisema, "Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Bwana Yesu Kristo." Toleo la King James lilisema, "katika Jina la Yesu Kristo"; bali katika *Emphatic Diaglott* linasema, "Katika Jina la Bwana Yesu Kristo."

180 Sasa, wakati nyinyi ndugu wa Umoja mnapobatiza tu katika Jina la Yesu, kuna Mayesu wengi; bali kuna mmoja tu...Yeye alizaliwa Kristo, Mwana wa Mungu. Yeye...Hilo ndilo Jina Lake, hivyo ndivyo Yeye alivyo. *Kristo* linamaanisha "aliyepakwa mafuta," Masihi, Kristo. Sasa, "Yesu," siku nane baadaye Yeye alipewa Jina, "Yesu," hapo alipotahiriwa. Naye ni Bwana wetu. Kwa hiyo Yeye ni Bwana wetu Yesu Kristo. Hivyo ndivyo alivyo.

181 Sasa, kuonyesha, mpate kuona ya kwamba Petro alikuwa na ufunuo ninaojaribu kuwaambia, sasa angalieni hivi—hivi vijisanduku upande huu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo Mathayo alivyosema. Siku kumi baadaye Petro alisema, "Bwana Yesu Kristo." Sasa, angalieni kama hizi sifa tatu si majina matatu, ama—ama, lile Jina moja la hizo sifa tatu.

182 Sasa, angalieni. Mathayo alisema, "Baba." Hiyo ni kweli? Nanii . . . Petro akasema, "Bwana." Sasa, Daudi alisema, "Bwana alimwambia Bwana Wangu." Sasa, wote wawili walisema jambo lile lile pale, sivyo? Vema, "Bwana wako . . . Bwana Mungu wako ni Mungu mmoja" ni kweli.

183 Vema, sasa, Petro alisema, "Katika Jina la Bwana," naye Mathayo akataja sifa ya Bwana huyo, ambayo ilikuwa ni "Baba." Bwana ni kile alicho, vema.

Mathayo alisema, "Mwana." Mwana ni nani? "Yesu," kasema Petro. Hiyo ni kweli?

Vema, sasa, naye Mathayo akasema, "Roho Mtakatifu." Petro akasema, "Kristo," ambaye ni Roho Mtakatifu, ile Logos iliyotoka kwa Mungu.

184 Mnaona? Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, ni Bwana Yesu Kristo, kitu hicho chote, hasa, Bwana Yesu Kristo. Kwa hiyo hizo ni sifa wala si . . . Haya basi.

Sasa, laiti tungalikuwa na muda mrefu zaidi, kuliingilia, lakini kunachelewa. Tunaweza kuinama, tuombe kwa muda kidogo tu?

185 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unajua ya kwamba hatujaribu kujaribu kusema jambo fulani hapa kumtatanisha mtu yeyote. Baba Mungu, tunajaribu kuondoa utata kutoka niani mwao. Wala hapana shaka kutakuwako na ndugu wahudumu Wakristo, wapendwa, wazuri, waaminio wa Utatu watakaousikia huu. Dada zetu huenda wakauchezea wachungaji wao. Nami ninaomba, Baba, ya kwamba—ya kwamba Wewe hutawaacha ndugu zangu wafikirie kwamba ninajaribu kutenda kama mjua yote ama kitu fulani. Lakini, Bwana, ninashukuru kwamba—kwamba Wewe umetupa ufunuo wa Neno.

186 Nami nimejaribu kuwa kama ndugu M—Mkristo kwao, kutolitaja kamwe miongoni mwa watu; kuendelea tu, kwa sababu, Bwana, ninaamini hao ni watoto Wako. Lakini wao—wao wanaona hizi zinazoonekana kama hitilafu katika Biblia, nao wamefanya hoja kuu kutoka kwake. Waassemblies wasingeshirikiana na wa Umoja; wa Umoja waliitwa . . . ambalo tunajua sasa, na hapa katika mkutano huu, wakishirikiana na baadhi ya hao ndugu. Nasi tunafanya hivyo katika kila mkutano.

187 Lakini, Bwana, tunajua hao wote ni watoto Wako, bali walifanya hoja kuu na kuondoka na kujitenga. Waassemblies hawatakuwa na uhusiano wowote nao, wala nao hawatakuwa na uhusiano wowote na Waassemblies na Churches of God, na kadhalika. Na kila mmoja, katika kufanya hivyo, Baba, ninatambua hao huchora mistari ya mipaka na kushikiza na kuunda dhehebu. Na Wewe ulifanya nini na madhehebu yote mawili? Uliyaweka kwenye rafu, nayo yote mawili yanakufa, na yamekufa kabisa.

188 Jalia watu wenye mioyo miaminifu waone, Bwana. Siwezi kuyafungua macho yao. Wewe Ndiwe pekee unayeweza kufanya hivyo. Ninaiwasilisha kweli Yako kwa ufunuo wa Yesu Kristo, ambao huyafunganisha maneno pamoja, Neno la Mungu, na kulifanya Neno la kweli. Ninaomba ya kwamba hawataelewa vibaya, bali watakupenda Wewe na kukutumikia Wewe siku zote za maisha yao, na kutembea katika Nuru. Tujalie, Bwana.

189 Ninawaombea wanawake hawa. Nami ninaomba ya kwamba kila mmoja atakayeuona huu, hautawafanya wachanganyikiwe, bali utawafanya waone njaa na kiu kwa ajili ya funuo zaidi za Mungu. Tujalie, Baba.

Naukabidhi huu Kwako sasa, Nawe ufanye nao lolote linaloonekana zuri mikononi Mwako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

61-0120 Ubatizo Wa Maji
Golden Arrow Restaurant
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org